# HABARI NJEMA *ya* FURAHA KUU

## MASOMO 25 YA KUTAFAKARI JUU YA KRISMASI

JOHN PIPER

**Vitabu vingine vilivyoandikwa na John Piper**

*Battling Unbelief*
*Bloodlines*
*Brothers, We Are Not Professionals*
*Coronavirus and Christ*
*The Dangerous Duty of Delight*
*Desiring God*
*Does God Desire All to Be Saved?*
*Don't Waste Your Life*
*Expository Exultation*
*Fifty Reasons Why Jesus Came to Die*
*Finally Alive*
*Five Points*
*Future Grace*
*God Is the Gospel*
*God's Passion for His Glory*
*A Godward Life*
*A Hunger for God*
*Lessons from a Hospital Bed*
*Let the Nations Be Glad!*
*A Peculiar Glory*
*The Pleasures of God*
*Providence*
*Reading the Bible Supernaturally*
*Seeing and Savoring Jesus Christ*
*Spectacular Sins*
*A Sweet and Bitter Providence*
*Taste and See*
*Think*
*Momentary Marriage*
*What Jesus Demands from the World*
*When I Don't Desire God*
*Why I Love the Apostle Paul*

# Habari Njema ya Furaha Kuu

*Masomo 25 ya Kutafakari juu ya Krismasi*

John Piper

EKKLESIA AFRIKA
BIBLICAL RESOURCES FOR BUILDING HEALTHY CHURCHES

**Toleo asili la Kiingereza:** ***Good news of Great Joy***
Hakimiliki © 2021 na Desiring God Foundation
Kimechapishwa na Crossway, Huduma ya Uchapishaji ya Good News Publishers
1300 Crescent Street, Wheaton, Illinois 60187
Haki zote kuhifadhiwa. Kutafsiriwa na kuchapishwa kwa idhini.
**Toleo la Kiswahili:** ***Habari Njema ya Furaha Kuu***
Hakimiliki © 2021 na Desiring God Foundation
Nakala hii imechapishwa kwa idhini ya The Ekklesia Afrika Ltd
P.O. Box 52861- 00100, Nairobi, Kenya
Kwa ushiriki wa mashirika ya Crossway na Desiring God Ministries.
**Tovuti:** www.ekklesiaafrika.org
Haki zote za kutafsiri, kuchapisha, kutohoa zimehifadhiwa
Kimetafsiriwa na BTL Kenya

BTL
Bible Translation & Literacy (E.A.)

Kimehakikishwa na Sakwa Buliba
**Muundo wa Jalada:** Picha ya Jalada

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili kitabu hiki wala kukihifadhi katika mfumo wowote ambao kinaweza kutolewa au kusambazwa tena kwa namna au njia yoyote ile, kwa kutolewa nakala, kurekodiwa, kutolewa fotokopi, au kwa mfumo wa kidijitali, elektroniki, au vinginevyo, bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapaji, isipokuwa kama inavyoelezwa katika sheria za hakimiliki za Kenya. The Ekklesia Afrika ni kampuni iliyosajiliwa nchini Kenya.

Nukuu zote za Maandiko zimechukuliwa kutoka Biblia ya® SUB (Swahili Union Version®), hakimiliki © 2001 na Crossway, huduma ya uchapishaji ya Good News Publishers Imetumiwa kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.

Nukuu za Maandiko zimechukuliwa kutoka SUV Swahili Union Version®.

Hakimiliki © 1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972, 1973, 1975, 1977, 1995 na The Lockman Foundation. Imetumiwa kwa ruhusa. www.Lockman.org. Mkazo wote katika nukuu za Maandiko umeongezwa na mwandishi.

**Jalada ngumu ISBN:** 978-1-4335-7323-1
**ePub ISBN:** 978-1-4335-7326-2
**PDF ISBN:** 978-1-4335-7324-8
**Mobipocket ISBN:** 978-1-4335-7325-5

# YALIYOMO


Dibaji *6*

Utangulizi: Yesu Anataka Nini Krismasi Hii? *12*

Siku ya 1 Tengeneza Njia (Luka 1:16–17) *18*

Siku ya 2 Mungu Mzuri wa Mariamu (Luka 1:46–55) *22*

Siku ya 3 Kujiwa Kulikongojewa Kwa Muda Mrefu (Luka 1:68–71) *26*

Siku ya 4 Kwa Watu Wanyonge wa Mungu (Luka 2: 1– 5) *30*

Siku ya 5 Hakuna Njia ya Mkato Kutoka Kalvari (Luka 2:6–7) *35*

Siku ya 6 Amani kwa Watu Ambao Mungu Amewaridhia (Luka 2: 12– 14) *39*

Siku ya 7 Masihi kwa ajili ya Majusi (Mathayo 2:1–2) *43*

Siku ya 8 Nyota ya Ajabu ya Bethlehemu (Mathayo 2:2) *47*

Siku ya 9 Aina Mbili za Upinzani Dhidi ya Yesu (Mathayo 2:3) *53*

Siku ya 10 Dhahabu, Uvumba, na Manemane (Mathayo 2:10 –11) *57*

Siku ya 11 Yesu Alikuja Kwa Nini? (Waebrania 2: 14– 15) *62*

Siku ya 12 Kuchukua Nafasi ya Mifano (Waebrania 8:1–2) *68*

Siku ya 13 Ukweli Halisi Uko Hapa (Waebrania 8:1–2, 5) *72*

Siku ya 14 Kuifanya Iwe Halisi Kwa Watu Wake (Waebrania 8:6) *76*

Siku ya 15 Uzima na Kifo Wakati wa Krismasi (Yohana 10:10) *81*

Siku ya 16 Unyonge wa Mungu Uliostawi Kabisa (Wafilipi 2:9–11) *86*

Siku ya 17 Wokovu Mkuu Zaidi Unaoweza Kufikirika (Yeremia 31: 31) *91*

Siku ya 18 Krismasi kama Kielelezo cha Uinjilisti (Yohana 17: 18) *96*

Siku ya 19 Krismasi ni ya Kukuweka Huru (Waebrania 2: 14– 15) *101*

Siku ya 20 Umoja wa Krismasi (1 Yohana 3:8) *106*

Siku ya 21 Kuzaliwa kwa Mwanzilishi wa Nyakati (Yohana 18: 37) *111*

Siku ya 22 Ndiposa Uweze Kuamini (Yohana 20:30–31) *116*

Siku ya 23 Zawadi ya Ajabu ya Mungu (Warumi 5: 10 – 11) *121*

Siku ya 24 Malengo Mawili ya Krismasi (1Yohana 3:7–8) *126*

Siku ya 25 Zawadi Tatu za Krismasi (1 Yohana 2:1–2; 3:7–8) *131*

Hitimisho: Maandiko yangu ya Krismasi Niyapendayo Zaidi *136*

Kiambatisho: Mifano ya Agano la Kale na Kuja kwa Kristo *142*

Faharasa ya Maandiko *146*

# Dibaji

Majira ya kuzaliwa kwa Kristo ni ya kumwabudu Yesu. Angalau huo ndio msimamo wetu katika shirika la "Desiring God".

Majira ya kuzaliwa kwa Kristo ni majira ya kila mwaka ya kungojea kwa ustahimilivu, matarajio yenye tumaini, kumtafuta Mungu, na kutazama kalenda inayokumbukwa na makanisa mengi, familia nyingi za Kikristo, na wafuasi binafsi wa Yesu. Hakuna amri ya kibiblia ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwa Kristo. Ni hiari—ni desturi iliyoendelezwa katika historia ya kanisa kama wakati wa kujitayarisha kwa ajili ya Siku ya Krismasi. Wengi wetu hujipata tunaadhimisha Krismasi kama tukio la kutuhimiza kiroho, kufurahia kiroho, na kutunufaisha kiroho.

Neno la Kiingereza *"advent"* linatokana na neno la Kilatini *"adventus"*, ambalo lina maana ya "kuja." The advent kimsingi kwa mtazamo wa kila Disemba ni kuingia Yesu duniani mara ya kwanza miaka elfu mbili iliyopita. Lakini kuja kwa Yesu mara ya pili pia huvutwa karibu, kama

wimbo maarufu wa Krismasi, "Furaha kwa Ulimwengu" huonyesha wazi wazi.

> Usiache tena dhambi na simanzi zikakua,
> Wala miiba kuijaza ardhi;
> Anakuja kufanya baraka zake zitiririke Mbali
> kufikia iliko laana.[1]

Shamrashamra hizi za Krismasi huanza Jumapili ya nne kabla ya tarehe 25 Disemba na huisha tarehe 25 jioni. Hili maana yake ni kwamba matayarisho haya huanza kama tarehe 27 Novemba hivi, ama ikichelewa tarehe 3 Disemba. Matayarisho ya Pasaka nayo huchukua takriban siku 40 hivi, zikiwa na Jumapili sita, ilhali Krismasi huchukua yapata kati ya siku 22 hadi siku 29 hivi.

Wakristo kote ulimwenguni wana njia zao tofauti za kusherehekea Majira ya Krismasi na mambo mbalimbali ya utendaji yanayodhihirika wakati huo. Wengine huwasha mishumaa. Wengine huimba nyimbo. Wengine hula vitafunio. Wengine hutoa zawadi. Wengine huning'iniza mashada ya maua. Wengi wetu hufanya haya yote.

Katika karne nyingi, tumeendeleza njia nyingi nzuri za kuongeza sherehe za kuzaliwa kwa Yesu. Zaidi ya hayo masaa

---

1 Isaac Watts, "Furaha kwa Ulimwengu," 1719.

mafupi ishirini na manne ya tarehe 25 Disemba. Kufanywa mwili kwa Mwana wa Mungu, "kwa ajili yetu na kwa ajili ya wokovu wetu," kama imani ya zamani inavyosema, ni shughuli muhimu sana ya kuadhimishwa kwa siku moja tu pekee. Naam, ni jambo ambalo tutasherehekea milele yote.

Ombi letu ni kwamba hiki kitabu kidogo cha kutafakari kiweze kukusaidia kumfanya Yesu awe azimio lako na hazina yako kuu zaidi ya majira yote. Mishumaa na vitafunio vina mahali pake lakini tunataka kuhakikisha kwamba katika misongamano yote ya Disemba tunamwabudu Yesu juu ya vitu vyote.

Kwa hivyo, "Njoni, tumuabudu" pengine ndiyo dhamira ya haya mafundisho juu ya Krismasi.[2] Tafakari hizi zote ni kuhusu kumwabudu Kristo, Bwana. Hapa na pale utasikia misemo ya "Njoo, Njoo, Imanueli," na mahali pengine "Waimba Sikizeni."[3] Na kwa hakika, tutakuwa na wito kutoka kwa majusi. Lakini picha kamili ni Yesu—mtoto mchanga aliyezaliwa Bethlehemu Mungu amefanyika mwanadamu akiwa amevalia nguo za kitoto, amelazwa horini, akielekezwa Kalvari, akiwa ametumwa na Baba yake ili afe na afufuke kwa ajili ya watu wake.

---

2 "Njoni Na Furaha," 1751 na John Francis Wade,

3 wa kupitia., "Njoo, Njoo, Imanueli," 1861; na John Mason Neale, "Waimba! Sikizeni Malaika." 1739, na Charles Wesley.

Utangulizi wa kitabu hiki umelengea kusomwa kabla ya Krismasi (au wakati wowote katika hayo majira). Hitimisho linaweza kusomwa kama chaguo la ziada Siku ya Krismasi (au wakati wowote kabla, hasa kama wewe unataka sana kujua kuhusu vifungu vya Maandiko vya Krismasi ambavyo Mchungaji John anavipenda zaidi). Kiambanisho juu ya mifano ya Agano la Kale na kuja kwa Kristo vinaambatana na Mafundisho ya sura ya ya 12 (na utapata maelezo katika mabano hapo).

Mungu na apendezwe kufanya kumwabudu Yesu kwenu Majira hayo ya Krismasi kuwe kwa kina zaidi na kwenye utamu zaidi.

David Mathis<br>
*Mhariri Mkuu*<br>
*Desiring God*

# *Utangulizi*

*Baba, hao ulionipa nataka wawe*
*pamoja nami po pote nilipo, wapate na kuutazama*
*utukufu wangu ulionipa; kwa maana ulinipenda kabla*
*ya kuwekwa msingi ulimwengu".*

Yohana 17:24

UTANGULIZI

# Yesu Anataka Nini Krismasi Hii?

Yesu anataka nini Krismasi hii? Tunaweza kuona jibu katika maombi yake. Anamwomba Mungu ampe nini? Maombi yake marefu zaidi yanapatikana katika Yohana 17. Kilele cha matamanio yake kiko katika kifungu cha 24.

Kati ya wenye dhambi wote wasiostahili ulimwenguni, kuna wale ambao Mungu "amempa" Yesu. Hawa ni wale ambao Mungu amewavuta na kuwaleta kwa Mwana (Yohana 6:44, 65). Hawa ni *Wakristo*—watu ambao *wamempokea* Yesu kama Mwokozi aliyesulubishwa na akafufuka, yeye ni Bwana na thamani ya maisha yao (Yohana 1:12; 3:17; 6:35; 10:11, 17–18; 20:28). Yesu anasema anataka wawe pamoja na yeye.

Wakati mwingine tunasikia watu wakisema kuwa Mungu alimuumba mwanadamu kwa sababu alikuwa na upweke. Kwa hivyo wanasema, "Mungu alituumba ili tuweze kuwa *pamoja na yeye*." Je, Yesu anakubaliana na

hilo? Kwa kweli anasema kwamba *anataka* tuwe pamoja na yeye! Ndio, lakini kwa nini? Angalia sehemu iliyosalia ya kifungu hiki. Kwa nini Yesu anataka tuwe pamoja na yeye?

> ...wapate na kuutazama utukufu wangu ulionipa (Baba) kwa maana ulinipenda kabla ya kuwekwa msingi ulimwengu.

Hiyo si njia ya kawaida ya kuonyesha upweke wake. “Nataka wawe pamoja nami wapate na kuutazama utukufu wangu.” Kwa kweli hili halionyeshi upweke wake. Linaonyesha jinsi anavyojali kutoshelezwa kwa hamu *yetu*, na sio upweke *wake*.

Yesu si mpweke. Yeye na Baba na Roho wanajitosheleza kwa kina kwa ushirika wa Utatu. Sisi ndio wenye njaa ya kitu fulani, si yeye. Na kile Yesu anachotaka kwa ajili ya Wakristo ni sisi tupate kile ambacho kwa kweli tuliumbwa kwa hicho—kuuona na kuufurahia utukufu wake.

Ee, Mungu na afanye hili lizame katika roho zetu! Yesu alitufanya (Yohana 1:3) tuuone utukufu wake.

Kabla hajaenda msalabani, Yesu anamwomba Baba tamanio lake la ndani kabisa: “Baba, hao ulionipa *natamani* [natamani!] kwamba... wawe pamoja nami popote nilipo, wapate na *kuutazama utukufu wangu.”*

Lakini hayo ni nusu peke yake ya kile ambacho Yesu anataka katika hivi vifungu vya mwisho vya jinsi mambo yalivyo vya maombi yake. Nimesema tu hivi punde sisi kwa kweli tumeumbwa kwa ajili ya kuuona na *kuufurahia* utukufu wake. Je, hicho ndicho anachotaka—kwamba licha ya kuuona utukufu wake pia tuufurahie, tuvutiwe nao, tupendezwe nao, tuuthamini, tuupende? Angalia kifungu cha 26, kifungu cha mwisho kabisa:

> Nami naliwajulisha jina lako, tena nitawajulisha hilo, *ili pendo lile ulilonipenda mimi liwe ndani yao,* nami niwe ndani yao.

Huu ndio mwisho wa hilo ombi. Lengo la Yesu la *mwisho* kwa ajili yetu ni lipi? Sio tu kwamba tuuone utukufu wake, lakini kwamba tumpende yeye na pendo lile lile alilo nalo Baba kwa ajili yake: "ili pendo lile ulilonipenda [Baba] liwe ndani yao."

Tamanio na lengo la Yesu ni kwamba tuuone utukufu wake, na kishaili tuweze kupenda kile tunachoona na pendo lile lile alilo nalo Baba kwa ajili ya Mwana. Na hamaanishi kwamba *tuige* tu lile pendo la Baba kwa ajili ya Mwana. Anamaanisha pendo lile lile la Baba hasa liwe pendo letu kwa ajili ya Mwana—kwamba tumpende Mwana na lile pendo la Baba kwa Mwana. Hivi ndivyo Roho anavyokuwa

na kutukirimia maishani mwetu:pendo la Baba kwa ajili ya Mwana kupitia kwa Roho.

Kitu anachotaka Yesu zaidi kwa ajili ya Wakristo ni kwamba wateule wake wakusanywe ndani na kisha *wao* wapate kile wanachotaka sana— *kuona* utukufu wake na kisha *waufurahie* na furaha ile ile hasa ya Baba kwa ajili ya Mwana.

Kile ninachotaka zaidi kwa ajili ya Krismasi mwaka huu ni kuungana na wewe (na wengine wengi) katika kumwona Kristo katika ukamilifu wake wote. Ili kwa pamoja tuweze kupenda kile tunachoona na pendo linalopita uwezo wetu wenyewe wa kibinadamu ulio wa moyo nusu nusu. Hili ndilo lengo letu katika mafundisho haya ya Krismasi. Tunataka kwa pamoja tumwone na kumfurahia huyu Yesu ambaye majira yake ya kwanza ya kuja (kuzaliwa) tunasherehekea, na ambaye tunangojea majira yake ya pili ya kuja.

Hivi ndivyo anavyotuombea Yesu Krismasi hii: Baba, waonyeshe utukufu wangu na uwape uwezo wa kupendezwa na mimi jinsi wewe unavyopendezwa na mimi." Ee, na sisi tuweze *kumwona* Kristo na macho ya Mungu na *tumfurahie* Kristo na moyo wa Mungu. Hiyo ndiyo asili ya mbingu. Hiyo ndiyo zawadi ambayo Yesu alikuja ili awanunulie wenye dhambi kwa gharama ya kufa kwa niaba yetu.

*Siku ya 1*

*Na wengi katika Waisraeli atawarejeza kwa Bwana Mungu wao.*
*Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya,*
*na nguvu zake,*
*ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto,*
*na kuwatilia waasi akili za wenye haki,*
*na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa.*

Luka 1:16–17

SIKU YA 1

# Tengeneza Njia

Majira ya Krismasi yanaweza kutufanyia kile ambacho Yohana Mbatizaji aliwafanyia Waisraeli. Usiache Krismasi ikupate ukiwa hujajitayarisha. Yaani kukosa kujitayarisha *kiroho*. Furaha yake na athari zake zitakuwa kuu zaidi kama ukiwa tayari!

Basi, ili uweze *kujitayarisha...*

Kwanza, tafakari juu ya ukweli kwamba tunahitaji *Mwokozi*. Krismasi inatuhukumu kabla haijaja furaha ya kusherehekea. Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, *Mwokozi*, ndiye Kristo Bwana" (Luka 2:11). Kama wewe hauna haja na Mwokozi, basi huna haja ya Krismasi. Krismasi haitaleta matokeo yaliyokusudiwa hadi pale tutakapohisi kiu ya kumhitaji Mwokozi. Mafundisho haya mafupi ya Krismasi na yakusaidie kuamsha ndani yako ari kali ndani yako ya kumhitaji Mwokozi.

Pili, jichunguze mwenyewe kwa busara kuhusu maana ya Krismasi kwakoIli Krismasi, ipewe tathmini sawa na ya

Pasaka, kusema, “Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu! / Unijaribu, uyajue mawazo yangu! / Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, / Ukaniongoze katika njia ya milele!” (Zaburi 139:23–24). Hebu kila moyo na *umtayarishie nafasi na kumkaribisha...* kwa kusafisha nyumba.

Tatu, jenga tumaini na matarajio na msisimko wa kumpendeza Mungu katika familia yako—hasa kwa watoto. Kama umesisimka kuhusu Kristo, hata hao nao watasisimka. Ikiwa unaweza kuifanya Krismasi iwe inasisimua tu na mapochopocho ya vitu pekee, watoto watapataje kiu ya Mungu? Elekeza jitihada zako kwa kuifanya ajabu ya kuja kwa mfalme iweze kuonekana kwa watoto.

Nne, zama zaidi katika Maandiko, na utafakari vifungu vikuu! “Je, neno langu si kama moto, Asema Bwana?” (Yeremia 23:29)! Kusanyikeni mkiuzunguka huo moto majira haya ya Krismasi. Kuna uchangamfu. Kunapatikana chemichemi za neema. Uponyaji wa majeraha makuu upo hapo. Ni nuru katika usiku wa giza.

*Siku ya 2*

*Moyo wangu wamwadhimisha Bwana,*
*Na roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu, kwa kuwa ameutazama unyonge wa mjakazi wake.*
*Kwa maana, tazama, tokea sasa Vizazi vyote wataniita mbarikiwa; kwa kuwa mwenye nguvu amenitendea makuu, na jina lake ni takatifu.*
*Na rehema zake hudumu vizazi hata vizazi kwa hao wanaomcha Amefanya nguvu kwa mkono wake; amewatawanya walio na kiburi katika mawazo ya mioyo yao;*
*amewaangusha wakuu katika viti vyao vya enzi na wanyonge amewakweza; wenye njaa amewashibisha mema, na wenye mali amewaondoa mikono mitupu.*
*Amemsaidia Israeli, mtumishi wake; ili kukumbuka rehema zake;*
*Kama alivyowaambia baba zetu, Ibrahimu na uzao wake hata milele.*

Luka 1:46-55

SIKU YA 2

# Mungu Mzuri wa Mariamu

Mariamu anaona wazi kabisa jambo lisilo na kifani kuhusu Mungu: yuko karibu kubadilisha mwelekeo wa hitoria yote ya mwanadamu; miongo mitatu muhimu zaidi katika nyakati zote iko karibu kuanza.

Je, Mungu yuko wapi? Anajishughulisha na wanawake wawili wanyonge, wasiojulikana—mmoja mzee na tasa (Elisabeti), mwingine msichana na bikira (Mariamu). Na Mariamu anaguzwa sana na haya maono ya Mungu, apendaye watu wadhaifu, kiasi kwamba anaanza kuimba—wimbo ambao umekuja kujulikana kama "Utenzi wa Mariamu."

Mariamu na Elisabeti ni mashujaa wazuri sana katika simulizi ya Luka. Anapendezwa sana na imani ya hawa wanawake. Jambo ambalo linamvutia zaidi, inaonekana, na jambo ambalo anataka limvutie Theofilo, msomi mheshimiwa wa Injili yake, ni hali ya chini na dhoofu

na uchangamfu wa Elisabeti na Mariamu wanapokuwa wanamtii Mungu wao mwema.

Elisabeti anasema (Luka 1:43), "Limenitokeaje neno hili, hata mama wa Bwana wangu anijilie mimi?" Na Mariamu anasema (Luka 1:48), "Ameutazama unyonge wa mjakazi wake."

Watu ambao roho zao zinaweza kumwadhimisha Bwana kwa kweli ni watu kama Elisabeti na Mariamu—watu ambao wanaukiri unyonge wao na wanafurahishwa na kujishusha chini kwa Mungu wao mwema.

# *Siku ya 3*

*Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli,*
*Kwa kuwa amewajia watu wake,*
*na kuwakomboa. Ametusimamishia pembe ya wokovu*
*Katika mlango wa Daudi,*
*mtumishi wake, kama alivyosema tangu mwanzo kwa*
*kinywa cha manabii wake watakatifu,*
*tuokolewe na adui zetu*
*Na mikononi mwao wote wanaotuchukia.*

Luka 1:68–71

SIKU YA 3

# Kujiwa Kulikongojewa Kwa Muda Mrefu

Tambua mambo mawili ya ajabu kutoka kwa maneno ya Zekaria, mumewe Elisabeti, katika Luka 1:68–71.

Kwanza miezi tisa kabla, Zekaria hakuamini kwamba mke wake angeweza kupata mtoto. Sasa, akiwa amejaa Roho Mtakatifu, amekuwa na uhakika sana na kazi ya Mungu ya wokovu kupitia kwa Masihi anayekuja hivi kwamba anaiweka katika njeo ya wakati uliopita: "Amewajia watu wake, na kuwakomboa." Kwani katika akili ya mwenye imani, kitendo kilichoahidiwa na Mungu huwa kimekwisha tendeka. Zekaria amejifunza kuamini kile asemacho Mungu na kwa hivyo ana hakikisho la ajabu: Mungu "amewajia na kuwakomboa!" (Luka 1:68).

Pili, kuja kwa Yesu Masihi ni kuja kwa Mungu katika ulimwengu wetu: *Mungu wa Israeli* amewajia

na kuwakomboa. Kwa karne nyingi, Wayahudi wamenyanyaswa kiasi kwamba wameamini kuwa Mungu aliwaacha: roho ya unabii ilikuwa imekoma, na Israeli ilikuwa imeanguka katika mikono ya Roma. Na watu wote wanaomcha Mungu kule Israeli walikuwa wanangojea kujiwa na Mungu. Luka anatwambia kwamba mzee mwingine, mcha Mungu Simeoni, alikuwa "akitarajia faraja ya Israeli!" (Luka 2:25). Vivyo hivyo, mwombezi aliyeitwa Ana alikuwa "akiutarajia ukombozi wa Yerusalemu" (Luka 2:38).

Hizi zilikuwa siku za matarajio makuu. Sasa, kuja kwa Mungu kulikongojewa kwa muda mrefu kuko karibu kufanyika—kwa kweli yuko karibu kuja katika njia ambayo hakuna mtu anayeitarajia.

*Siku ya 4*

*Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba*
*iandikwe orodha ya majina ya watu*
*wote wa ulimwengu.*
*Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyoandikwa hapo Kirenio*
*alipokuwa liwali wa Shamu.*
*Watu wote wakaenda kuandikwa, kila mtu mjini kwao.*
*Yusufu naye aliondoka Galilaya, toka mji wa Nazareti,*
*akapanda kwenda Uyahudi mpaka mji wa Daudi,*
*uitwao Bethlehemu, kwa kuwa yeye ni wa mbari na*
*jamaa ya Daudi, ili aandikwe pamoja na Mariamu*
*mkewe, ambaye amemposa, naye ana mimba.*

Luka 2:1–5

SIKU YA 4

# Kwa Watu Wanyonge wa Mungu

Je, umewahi kufikiri jinsi inavyoshangaza kwamba Mungu alipanga kimbele kwamba Masihi azaliwe Bethlehemu (kama unabii katika Mika 5:2 unavyoonyesha)? Na je, unashangaa kwamba alipanga mambo ambayo wakati ulipofika, mama wa Masihi na baba wa kisheria walikuwa hawaishi Bethlehemu bali walikuwa wanaishi Nazareti. Na kwamba ili atimize neno lake, na kuwaleta watu wawili wasiojulikana, wasiokuwa na jina tajika, watu wanyonge, waje Bethlehemu hiyo Krismasi ya kwanza. Mungu aliweka katika moyo wa Kaisari Augusto kwamba watu wote katika nchi zote zilizo chini ya utawala wa Kirumi wanapaswa waandikishwe katika miji yao wenyewe. Amri hii ilikuwa kwa manufaa ya ulimwengu wote ili aweze kuwapeleka watu wawili (Mariamu na Yosefu) maili sabini!

Je, umewahi kujihisi, kama mimi, kuwa mtu mdogo na duni katika ulimwengu wa takriban watu bilioni saba, ambapo habari zote zinahusu vyama vikubwa vya kisiasa

na habari motomoto za kiuchumi na kijamii na watu maarufu na muhimu ulimwenguni kote, wenye uwezo mwingi na sifa nyingi? Kama umewahi kuhisi namna hiyo, hilo lisikufanye wewe uvunjike moyo au ukose furaha. Kwa maana inadokezwa katika Maandiko kwamba nguvu zote kuu za kisiasa na changamoto zote kuu za kitasnia, bila hizo zenyewe kujua, zinaelekezwa moja kwa moja na Mungu. Zinaelekezwa si kwa ajili yao wenye sifa, bali kwa ajili ya watu wanyonge wa Mungu—watu wadogo kama Mariamu na Yusufu ambao wanalazimika kutoka Nazareti hadi Bethlehemu. Mungu anatumia utawala mkuu kutimiza neno lake na kubariki watoto wake.

Usifikiri kwamba kwa sababu unapata upinzani katika ulimwengu wako mdogo wa uzoefu, mkono wa Bwana umefupika. Si ufanisi wetu wala umaarufu wetu wa kidunia bali ni utakatifu wetu ambao Mungu anatafuta kuafikia. Na kwa hatima hiyo, anatawala ulimwengu wote. Kama Mithali 21:1 isemavyo, "Moyo wa mfalme huwa katika mkono wa Bwana; / kama mifereji ya maji huugeuza popote apendapo." Na anaugeuza siku zote kwa ajili ya malengo yake ya milele ya kuwaokoa na kuwatakasa watu wake.

Yeye ni Mungu mkuu kwa ajili ya watu wadhaifu, na tuna sababu kuu ya kufurahi kwamba, bila wao kujua, wafalme wote na maraisi na mawaziri wakuu na wakuu wa

serikali na machifu wa ulimwengu hufuata amri za kifalme za Baba yetu aliye Mbinguni. Inakuwa hivyo, ili sisi watoto wake tuweze kuiga na tufanane na mfano wa Mwanawe, Yesu Kristo—na kisha tuingie utukufu wake wa milele.

# *Siku ya 5*

*Ikawa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia. Akamzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.*

Luka 2:6–7

SIKU YA 5

# Hakuna Njia ya Mkato Kutoka Kalvari

Unaweza kufikiri kwamba, kama Mungu kweli anatawala ulimwengu na anaweza kutumia sensa ya utawala mzima kumleta Mariamu na Yusufu Bethlehemu, hakika angeweza kuhakikisha kwamba kulikuwa na chumba katika nyumba ya wageni.

Ndio, angeweza kuhakikisha hilo. Angeweza kuhakikisha hilo kabisa! Pengine Yesu *angekuwa* amezaliwa katika jamaa ya matajiri, *angekuwa* amegeuza jiwe likawa mkate kule nyikani. Huenda *angekuwa* ameita malaika elfu kumi waje wamsaidie kule Gethsemane. Labda *angekuwa* ameshuka kutoka msalabani na kujiokoa mwenyewe. Swali si kile ambacho Mungu *angekuwa* kufanya, bali kile ambacho *alikusudia* kufanya.

Mapenzi ya Mungu yalikuwa, ingawa Kristo alikuwa tajiri, lakini *kwa ajili ya* wanyonge alifanyika kuwa

maskini. Ilani za "Hakuna Nafasi" katika hoteli zote kule Bethlehemu zilikuwa kwa ajili yako. "Kwa *ajili yako* alikuwa maskini" (2 Wakorintho 8:9).

Mungu anatawala vitu vyote—hata nafasi za hoteli na kuwako kwa vyumba vya kukodisha—kwa ajili ya watoto wake. Njia ya Kalvari inaanza na ilani ya "Hakuna Nafasi" kule Bethlehemu na inaisha na kutemewa mate na kudhihakiwa pale msalabani, Yerusalemu.

Na tusisahau kwamba Yesu alisema: "Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate." (Luka 9:23). Tunaungana naye katika njia ya Kalvari na kumsikia akisema, "Likumbukeni lile neno nililowaambia; 'Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake.' Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi" (Yohana 15:20).

Kwa yule anayemwita kwa hamu, "Nitakufuata ko kote utakakokwenda," Yesu anamjibu, "Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana pa kujilaza kichwa chake" (Luka 9:57–58).

Ndio, Mungu angekuwa amehakikisha kwamba Yesu anapata chumba wakati wa kuzaliwa kwake. Lakini huko kungekuwa kutoka nje ya njia ya Kalvari.

*Siku ya 6*

*"Na hii ndiyo ishara kwenu: mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe." Na mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema,"Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia!"*

Luka 2:12–14

SIKU YA 6

# Amani kwa Watu Ambao Mungu Amewaridhia

Amani kwa ajili ya nani? Kuna onyo zito katika sifa za wale malaika. Amani kati ya wale ambao neema yake iko juu yao. Amani kati ya wale aliowaridhia. Lakini pasipo imani, haiwezekani kumpendeza Mungu (Waebrania 11:6). Kwa hivyo, Krismasi haileti amani kwa watu wote.

"Hii ndiyo hukumu," Yesu alisema, "nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru, kwa maana matendo yao yalikuwa maovu" (Yohana 3:19). Au kama mzee Simeoni alivyosema alipomwona mtoto Yesu, "Tazama, huyu amewekwa kwa kuanguka na kuinuka wengi walio katika Israeli, na kuwa ishara itakayonenewa... ili yafunuliwe mawazo ya mioyo mingi" (Luka 2:34–35). Ee, kuna wangapi ambao wanatazamia siku ya Krismasi

isiyokuwa na misisimko na hawataona zaidi ya hiyo—kwamba kuna ishara ya kupingwa.

"Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu ndio wale *waliaminio* jina lake" (Yohana 1:11–12). Yesu alisema tu kwa wanafunzi wake peke yake, "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa. Niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga." (Yohana 14:27).

Watu wanaofurahia amani ya Mungu ipitayo ufahamu wote ni wale ambao katika kila neno kwa kusali na kuomba na kufanya haja zao zijulikane na Mungu (Wafilipi 4:6–7).

Ufunguo unaofungua sanduku la hazina la amani ya Mungu ni amani katika ahadi za Mungu. Kwa hivyo, Paulo anaomba, "Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika *kuamini*" (Warumi 15:13). Na *tunapoamini* ahadi za Mungu na kuwa na furaha na amani na upendo, basi Mungu anatukuzwa.

Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kati ya wale aliowaridhia! Kila mtu—kutoka kila tabaka, lugha, kabila, na taifa—atakayeamini.

## *Siku ya 7*

*Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu, wakisema, "Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi?"*

Mathayo 2:1–2 (SUV)

SIKU YA 7

# Masihi kwa ajili ya Majusi

Tofauti na Luka, Mathayo hatwambii kuhusu wachungaji kuja kumwona Yesu katika hori. Mara moja msisitizo wake uko juu ya wageni—Mataifa, watu ambao si Wayahudi —kuja kutoka mashariki ili wamwabudu Yesu.

Kwa hivyo, Mathayo anamwasilisha Yesu mwanzoni na mwishoni mwa Injili yake kama Masihi kwa watu wote kwa ajili ya mataifa yote - si kwa ajili ya Wayahudi pekee.

Hapa watu wa kwanza kumwabudu ni waganga katika nyumba za kifalme, au majusi, au watu wenye hekima, si wa kutoka Israeli bali kutoka mashariki—pengine kutoka Babeli. Walikuwa watu wa mataifa. Hii ilikuwa najisi, kulingana na sheria za dini za Agano la Kale.

Na mwisho wa Mathayo, maneno ya mwisho ya Yesu ni, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi" (Mathayo 28:18–19).

Maneno haya yalitupatia sisi watu wa mataifa fursa ya kumfurahia Masihi na pia kuongeza uthibitisho kwamba yeye alikuwa Masihi. Hili ni kwa sababu unabii mmoja ambao umenenwa tena na tena ni kwamba mataifa na wafalme kwa kweli wangemjia yeye kama mfalme wa ulimwengu. Kwa mfano, Isaya 60:3:

> Na mataifa wataijilia nuru yako,
> na wafalme kuujia mwanga wa kuzuka kwako.

Kwa hivyo, Mathayo anaongeza uthibithisho kuwa Yesu ni Masihi *na* anaonyesha kuwa yeye ni Masihi— mfalme, na mtimizaji wa ahadi—kwa ajili ya mataifa yote, si Israeli peke yake.

*Siku ya 8*

*Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake ilipotokea kule mashariki nasi tumekuja kumsujudia.*

Mathayo 2:2

SIKU YA 8

# Nyota ya Ajabu ya Bethlehemu

Kila mara Biblia inatufanya tuchanganyikiwe tunapotaka kujua kuhusu jinsi mambo fulani yalivyofanyika. Hii "nyota" iliwaletaje wale majusi kutoka mashariki mpaka Yerusalemu?

Haisemi kwamba iliwaongoza au iliwatangulia njiani mpaka Yerusalemu. Biblia inasema tu kwamba waliona nyota kule mashariki (Mathayo 2:2) na wakaja Yerusalemu. Na hiyo nyota iliwatangulia namna gani katika huo mwendo mdogo wa maili tano kutoka Yerusalemu hadi Bethlehemu kama Mathayo 2:9 inavyosema? Ni kwa namna gani hiyo nyota "ilisimama juu mahali alipokuwapo mtoto"?

Jibu ni kwamba hatujui. Kuna jitihada nyingi za kueleza hilo kwa kutumia viunganishi vya sayari au vimondo au supanova au mianga ya kimiujiza. Sisi hatujui. Ningependa kukusihi usiwe mtu wa kukisia na kubahatisha mambo ukitumia nadharia ambazo hazina mashiko wala umuhimu wowote wa kiroho.

Ningependa kukushauri na kukuonya kwamba watu wenye jitihada za kukisia na kutabiria mambo kama vile nyota ilifanya kazi na jinsi Bahari ya Shamu ilivyogawanyika, na jinsi mana ilivyoanguka kutoka mbinguni, na jinsi Yona alivyoendelea kuishi baada ya kumezwa na samaki, na jinsi mwezi unavyogeuka kuwa damu, kwa hakika ni watu ambao wana fikira za kijuujuu.

Ndani yao huwezi kuona utunzaji wa kina wa mambo makuu ambayo ndiyo nguzo ya injili: utakatifu wa Mungu, uovu wa dhambi, kutojitosheleza kwa mwanadamu, kifo cha Kristo, kuhesabiwa haki kupitia kwa imani pekee yake, kazi ya utakaso inayofanywa na Roho, utukufu wa kurudi kwa Kristo, na hukumu ya mwisho. Siku zote wanaonekana kujaribu kupotezea wengine njia na makala mapya au kitabu kinachowasisimua, kinachoshughulikia jambo geni. Hawapati msisimko na mambo halisi na makuu ambayo ndiyo nguzo ya imani.

Kile ambacho kiko wazi kuhusu tukio la nyota ni kwamba nyota inaonekana kufanya kitu ambacho haiwezi kukifanya kwa uwezo wake kama nyota: inawaongoza majusi mpaka wanafika kwa Mwana wa Mungu ili wamwabudu. Kuna mmoja pekee katika mtiririko wa mawazo ya kibiblia ambaye anaweza kuwa chanzo cha nyota kutekeleza jukumu hili: Mungu mwenyewe. Kwa hivyo, somo liko wazi: Mungu anawaelekeza wageni mpaka kwa Kristo ili

wamwabudu. Anafanya hivyo kwa kusababisha kuweko kwa uwezo na nguvu za ajabu ulimwenguni—yamkini hata za kutikiza vitu vyote—ilimuradi kusababisha jambo hilo litendeke.

Luka anamwonyesha Mungu akielekeza Utawala wote wa Roma. Alifanya hivi ili ndiposa sensa ifanyike wakati ule ule wa kumpeleka msichana bikira asiyejulikana kokote, aende Bethlehemu kutimiza unabii na kuzaa Mwana atakayeokoa ulimwengu. Mathayo anamwonyesha Mungu akielekeza nyota za angani ili ziwalete wageni kule Bethlehemu ili waweze kumwabudu Mwana.

Huu ni mpango wa Mungu. Alifanya hivyo wakati huo. Na hata sasa bado anafanya hivyo. Lengo lake ni kwamba mataifa—mataifa yote (Mathayo 24:14)—yamwabudu Mwana.

Haya ndiyo mapenzi ya Mungu kwa ajili ya kila mtu katika ofisi yako kule kazini na katika darasa lako na katika eneo lako na nyumbani kwenu. Kama Yohana 4:23 kisemavyo, "Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu."

Mwanzoni mwa Injili ya Mathayo bado kuna mwaliko wa, "njoni muone". Lakini mwishoni mwa kitabu cha Mathayo, ujumbe ni, "nendeni mkawaambie." Wale majusi walikuja wakaona. Sisi tunapaswa kwenda na kutangaza yale tumeona na kusikia.

Kile ambacho hakibadiliki ni lengo na uwezo wa Mungu katika kukusanya mataifa yote ili wamwabudu Mwanawe. Kumtukuza Kristo kwa kumwabudu na kumsujudia kwa mataifa yote ndiyo sababu ya ulimwengu kuwako.

# *Siku ya 9*

*Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye.*

Mathayo 2:3

SIKU YA 9

# Aina Mbili za Upinzani Dhidi ya Yesu

Yesu huwafadhaisha watu ambao hawataki kumwabudu, na huchochea upinzani dhidi ya wale wanaomwabudu. Yamkini hili sio wazo kuu katika akili ya Mathayo, lakini ni kidokezi ambacho hatuwezi kukiepuka hadithi hii inapoendelea.

Katika hadithi hii, kuna watu wa aina mbili ambao hawataki kumwabudu Yesu.

Aina ya kwanza ni watu ambao hawafanyi lolote kumhusu Yesu. Yeye si lolote, si chochote maishani mwao. Kundi hili linawakilishwa mwanzoni mwa maisha ya Yesu na makuhani wakuu na waandishi. Mathayo 2:4 inasema, "Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, [Herode] akatafuta habari kwao, Kristo azaliwa wapi." Basi wakamwambia, na ikaishia hapo: wakaendelea na shughuli zao za kawaida. kimya hicho tu na kutofanya

lolote kwa viongozi vinashangaza sana ukitazama umaarufu wa yale yaliyokuwa yanafanyika.

Na tambua kwamba Mathayo 2:3 inasema, "Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye." Kwa maneno mengine, kulikuwa na tetesi zilizokuwa zinaenea kwamba mtu fulani alikuwa anafikiri Masihi amezaliwa. Kutofanya lolote kwa makuhani wakuu kunashangaza: kwa nini hawakuenda na wale majusi? Hawavutiwi na lolote. Hawana ari ya kumtafuta Mwana wa Mungu na kumwabudu.

Aina ya pili ya watu ambao hawataki kumwabudu Yesu ni wale watu ambao katika kilindi cha mioyo yao wametishwa na yeye. Huyo ni Herode katika hadithi hii. Kwa kweli ameogopa sana—hivi kwamba anapanga na kufanya hila kwa kuua watoto wengi kwa pamoja ili aweze kumwangamiza Yesu.

Kwa hivyo leo, hizi aina mbili za upinzani zitakuja dhidi ya Kristo na watu wake wanaomwabudu: ubaridi na uhasama. Kwa hakika natumaini kwamba wewe haumo katika mojawapo ya makundi haya mawili.

Ikiwa wewe ni Mkristo, hebu acha Krismasi hii iwe wakati wa wewe kutafakari maana yake—yaani inagharimu nini kumwabudu na kumfuata huyu Masihi.

*Siku ya 10*

*Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno. Wakaingia nyumbani, wakamwona Mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia. nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu na uvumba na manemane.*

Mathayo 2:10–11 (SUV)

SIKU YA 10

# Dhahabu, Uvumba, na Manemane

Mungu hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu chochote (Matendo 17:25). Zawadi za majusi hazitolewi kwa lengo la kusaidia au kana kwamba kuna wenye mahitaji. Jambo hili lingemvunjia heshima mfalme kama wageni wangekuja na matoleo yanayonuia kumsaidia mfalme.

Vilevile zawadi hizi hazikuwa za kulipa hongo. Kumbukumbu la Torati 10:17 inasema kwamba Mungu hakubali rushwa. Kwa hivyo, maana ya zawadi hizi ni nini? Zinakuwaje za kuonyesha Masihi anaabudiwa?

Zawadi zinazotolewa kwa watu matajiri, wanaojitosheleza huonyesha taathima walio nayo na kuhdihirisha jinsi mtoaji anavyomuenzi anayepokezwa vipaji hivyo. Kwa maana fulani, kumtolea zawadi Kristo ni kama kufunga—kwenda bila kula chochote kwa muda

ili uonyeshe kwamba Kristo ana thamani zaidi kuliko chakula.

Unapomtolea zawadi Kristo namna hii, ni njia ya kusema, "Furaha ninayoitafuta [kumbuka Mathayo 2:10! "Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno"]. si tumaini la kuwa tajiri kwa kubadilishana vitu na wewe au kuelewana malipo fulani. Nimekuja kwako si kwa ajili ya *vitu* vyako bali kwa ajili yako *wewe mwenyewe*. Tamanio hili sasa ninaliongeza na kulidhihirisha kwa kutoa *vitu* nikitumaini kwamba nitakufurahia wewe zaidi. Kwa kukupatia kile ambacho haukihitaji na kile ambacho ninaweza kufurahia, ninasema kwa dhati na kwa uhakika kwamba, 'Wewe ndiwe wa thamani kwangu, wala sio hivi vitu.'

Nafikiri hiyo ndiyo maana ya kumwabudu Mungu kwa vipawa, dhahabu, uvumba, na manemane. Au chochote kile kingine tunachoweza kufikiri kumpa Mungu.

Mungu na aamshe hamu ndani yetu kwa ajili ya Kristo mwenyewe. Na tuseme kutoka moyoni, "Bwana Yesu, wewe ndiwe Masihi, Mfalme wa Israeli. Mataifa yote yatakuja na kusujudu mbele yako. Mungu anatumia ulimwengu kuhakikisha kwamba unaabudiwa. Kwa hivyo, hata nipate upinzani wa namna gani, kwa furaha ninakiri kwamba mamlaka na heshima ni vyako, na ninaleta zawadi

zangu kusema kwamba wewe peke yako ndiwe uwezaye kutosheleza moyo wangu."

*Siku ya 11*

*Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa.*

Waebrania 2:14–15

SIKU YA 11

# Yesu Alikuja Kwa Nini?

Waebrania 2:14-15 nafikiri ndiyo maandiko ninayopenda zaidi kuhusu Krismasi. Hii ni kwa sababu sijui kifungu kingine cha Biblia kinachoonyesha bayanauhusiano uliopo kati ya mwanzo na mwisho wa maisha ya Yesu hapa duniani—yaani kati ya kufanyika kuwa mwili na kusulubishwa. Hivi vifungu viwili vinaeleza wazi Yesu alikuja kwa nini, kwamba alikuja ili afe. Vinaweza kuwa vifungu muhimu sana kutumia na marafiki wasioamini au watu wa familia kwenda nao hatua kwa hatuakupitia mtazamo wako wa Kikristo kuhusu Krismasi. Inaweza kwenda namna hii, hatua kwa hatua:

> Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili…

Neno "watoto" linachukuliwa kutoka katika kifungu kilichotangulia (Waebrania 2:13) na linasema kuhusu

uzao wa kiroho wa Kristo, Masihi (tazama Isaya 8:18; 53:10). Hawa pia ni "watoto wa Mungu" (Yohana 1:12). Kwa maneno mengine, katika kumtuma Kristo, Mungu anauatazamia wokovu wa "watoto" wake.

Ni kweli kwamba "Mungu aliupenda *ulimwengu*, hata akamtoa [Yesu]" (Yohana 3:16). Lakini pia ni kweli kwamba Mungu alikuwa *haswa* anakusanya "watoto wa Mungu waliotawanyika kote" (Yohana 11:52). Mpango wa Mungu ulikuwa *kumtoa* Kristo kwa ulimwengu na ili *aufanikishe* wokovu wa watoto wake (tazama 1 Timotheo 4:10). Unaweza kufanywa mwanawe kwa kumpokea Kristo (Yohana 1:12).

> ...yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, [mwili na damu]...

Hili linamaanisha kwamba Kristo alikuwako kabla ya kufanywa mwili. Alikuwa roho. Alikuwa Neno la milele. Alikuwa na Mungu na palikuwa Mungu (Yohana 1:1; Wakolosai 2:9). Lakini alichukua mwili na damu, na akajivika uungu na uanadamu. Alikuwa mwanadamu kamili na akabaki kuwa Mungu kamili. Ni hali ngumu yetu sisi kuelewa kwa namna ilivyokuwa. Lakini hiki ndicho kitovu cha imani yetu—na kile ambacho Biblia inafundisha.

> ...kwamba kupitia kwa kifo...

Sababu iliyomfanya awe mwanadamu ni ili afe. Kama Mungu kamili na kawaida, hangeweza kufa kwa ajili ya wenye dhambi. Lakini kama mwanadamu

Angeweza kusulubiwa na kufa. Lengo lake lilikuwa afe kwa ajili ya wenye dhambi. Kwa hivyo, ilikuwa ni lazima azaliwe mwanadamu. Alizaliwa ili afe. Siku ya Ijumaa aliposulubiwa ndilo lililokuwa lengo la Krismasi (kuzaliwa kwake). Hili ndilo ambalo watu wengi wanahitaji kusikia leo kuhusu maana ya Krismasi.

> ...amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti,
> yaani, ibilisi...

Katika kufa, Kristo alimng'oa meno ibilisi. Kwa namna gani? Kwa kusafisha dhambi zetu zote. Hili linamaanisha kwamba shetani hana sababu za kutushitaki mbele ya Mungu. "Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki" (Warumi 8:33)—anawahesabia haki kwa sababu gani? Kupitia kwa damu ya Yesu (Warumi 5:9).

Silaha ya kimsingi ya shetani ni dhambi zetu wenyewe. Kama kifo cha Yesu kinaiondoa, silaha kuu ya ibilisi—silaha moja ya kuua aliyo nayo—inatolewa katika mkono

wake. Hawezi kuwa na kesi yoyote ya kutufanya sisi tupate hukumu ya kifo, kwa sababu Hakimu ametuacha huru kwa kifo cha Mwanawe!

> ...awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa.

Kwa hivyo tuko huru kutoka kwa hofu ya mauti. Mungu ametuhesabia haki. Shetani hawezi kugeuza hiyo amri. Na Mungu anataka kwa ajili ya usalama wetu *kamili* amri hiyo iweze kuleta matokeo yaliyokusudiwa *mara moja* juu ya maisha yetu.Anataka hatima yenye furaha iondoe utumwa na hofu ya wakati huu.

Kama hatuna haja ya kuwa na hofu ya adui wetu wa mwisho na mkubwa zaidi, mauti, basi hatuna haja ya kuwa na hofu na kitu chochote. Tunaweza kuwa huru. Kuwa huru kwa ajili ya furaha. Kuwa huru kwa ajili ya wengine.

Hii ni zawadi kubwa sana ya Krismasi, kutoka kwa Mungu kuja kwetu! Na kutoka kwetu hadi kwa ulimwengu!

*Siku ya 12*

*Basi, katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili: Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni, mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu.*

Waebrania 8:1–2 (SUV)

SIKU YA 12

# Kuchukua Nafasi ya Mifano

Wazo la kitabu hiki cha Waebrania ni kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, hakuja kuingiliana tu na mfumo wa kidunia wa huduma ya ukuhani kama kuhani mwanadamu wa mwisho na bora zaidi. Alikuja kutimiza na kukomesha huo mfumo na kuuelekeza usikivu wetu wote kwake yeye, akituhudumia mara ya kwanza pale Kalvari kama sadaka yetu ya mwisho na kisha kule mbinguni kama kuhani wetu wa mwisho.

Hema ya Agano la Kale na makuhani na sadaka vilikuwa mifano. Sasa kilicho halisi kimekuja, na mifano imepita.

Hapa kuna kielelezo cha Krismasi kwa ajili ya watoto—na wale kati yetu waliokuwa watoto na wanaokumbuka kuwa mtoto kulivyokuwa. Tuseme wewe na mamako mpotezane kule dukani na uanze kuogopa na kuwa na wasiwasi. Hujui utashika njia gani, na ukimbie mpaka mwisho wa hiyo njia katika hilo duka. Kabla hujaanza kulia, uone kivuli sakafuni hapo mwisho wa hiyo njia,

ambacho kimefanana na mamako. Kinakufanya uwe na tumaini kweli kweli. Lakini kilicho bora ni kipi? Tumaini ulilo nalo la kuona kivuli, au kumwona mamako kwa kweli akijitokeza kule pembeni?

Hivyo ndivyo ilivyo wakati Yesu anapokuja na kuwa kuhani wetu mkuu. Hivyo ndivyo Krismasi ilivyo. Krismasi ni kitu halisi kuchukua nafasi ya mifano: Mama kujitokeza pembeni mwa hiyo njia pamoja na afueni yote na furaha anayoweza kumpa huyo mtoto. (Kwa taarifa zaidi kuhusu jinsi kuja kwa Kristo kunachukua nafasi ya Agano la Kale, tazama kiambatisho mwisho wa kitabu hiki).

# *Siku ya 13*

*Basi, katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili: Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni, mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu... Watumikiao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni. Kama Musa alivyoagizwa na Mungu, alipokuwa tayari kuifanya ile hema; maana asema, "Angalia ukavifanye vitu vyote kwa mfano ule ulioonyeshwa katika mlima."*

Waebrania 8:1–2, 5

SIKU YA 13

# Ukweli Halisi Uko Hapa

Jinsi tumeona hapo awali. Kuna maelezo zaidi. Krismasi ni tukio halisia la kuchukua mahala pa mifano. Waebrania 8:1–2, 5 ni kama muhtasari wa maelezo. Neno kuu ni kwamba yule Kuhani aliye kati yetu na Mungu anayetupatanisha na Mungu na kutuombea kwa Mungu si Kuhani wa kawaida, mnyonge, mwenye dhambi, kuhani afaye kama siku za Agano la Kale. Yeye ni Mwana wa Mungu—mwenye nguvu, hana dhambi, ana maisha yasiyoharibika.

Si hayo tu, kwani yeye hahudumu katika hema la dunia lililo na upungufu, udhoofu, linachakaa na kuliwa na nondo na kulowa na kuchomwa na kuraruka na kuibwa. Hasha, Waebrania 8:2 inasema kwamba Kristo anahudumu kwa ajili yetu katika "hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu." Huu si mfano, picha wala kivuli kama vya Agano la Kale. Hii ni hali halisi kule mbinguni.

Huu ni ule uhalisi ulioweka mfano pale juu ya Mlima wa Sinai ili Musa apate kuufuata.

Kulingana na Waebrania 8:1, kitu kingine kikubwa kuhusu ule uhalisia ambao ni mkuu kuliko kile kivuli ni kwamba Kuhani wetumkuu amekaa mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu kule mbinguni. Hakuna kuhani wa Agano la Kale ambaye angeweza kusemwa hivyo. Yesu anafanya kazi moja kwa moja na Mungu Baba. Ana nafasi ya heshima karibu na Mungu. Anapendwa na kuheshimiwa na Mungu bila kikomo. Yeye yuko na Mungu kila mara. Hiki si kivuli cha uhalisia kama vile pazia na vibakuli na meza na mishumaa na na kanzu na mashada na kondoo na mbuzi na njiwa. Huu ni uhalisi wa mwisho na mkamilifu: Baba na Mwanawe wakiingiliana kwa upendo na utakatifu kwa ajili ya wokovu wetu wa milele.

Uhalisi mkamilifu ni nafsi za Mungu katika uhusiano, kufanya kazi pamoja kuhusu jinsi ukuu wao na utakatifu na upendo na haki na wema na ukweli utakavyodhihirishwa ndani ya watu waliokombolewa.

# *Siku ya 14*

*Lakini sasa amepata huduma iliyo bora zaidi, kwa kadiri alivyo mjumbe wa agano lililo bora, lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora.*

Waebrania 8:6

SIKU YA 14

# Kuifanya Iwe Halisi Kwa Watu Wake

Kristo ndiye mjumbe wa Agano Jipya kulingana na Waebrania 8:6: Hilo lina maana gani? Linamaanisha kwamba damu yake—damu ya agano (Luka 22:20; Waebrania 13:20)—hatimaye na kwa kuamua ilinunua na kupata hakikisho la kutimizwa kwa ahadi za Mungu kwa ajili yetu.

Inamaanisha kwamba Mungu, kulingana na hizo ahadi za Agano Jipya, hutuletea mabadiliko ya ndani kupitia kwa Roho wa Kristo.

Na inamaanisha kwamba Mungu hufanya haya mabadiliko ndani yetu kupitia kwa imani—imani katika yote ambayo Mungu amenena kwetu katika Kristo.

Agano Jipya linanunuliwa na *damu* ya Kristo, linatekelezwa na *Roho* wa Kristo, na kupatikana kwa *imani* katika Kristo. Mahali pazuri zaidi pa kumwona Kristo

akifanya kazi kama mjumbe wa Agano Jipya ni katika Waebrania 13:20–21.

> Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake, naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake… *kupitia kwa Yesu Kristo*, utukufu una yeye milele na milele. Amen.

Maneno "akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake…" yanaeleza kile ambacho hufanyika wakati Mungu anapoandika sheria kwenyemioyo yetu kulingana na agano jipya. Na manenov "kwa Yesu Kristo" yanamweleza Yesu kama mjumbe wakazi hii tukufu ya neema kuu.

Kwa hivyo, maana ya Krismasi si tu kwamba Mungu anachukua nafasi ya mifano na kuweka uhalisia, lakini pia kwamba anachukua uhalisia na kuufanya uwe halisi kwa watu wake. Anauandika mioyoni mwetu. Haweki zawadi yake ya Krismasi, ya wokovu na mabadiliko chini ya mti, kitu kama hicho, ili wewe uweze kuokota tu kwa nguvu zako mwenyewe. Anaichukua na kuitiamoyoni mwako na

akilini mwako na kukuwekea mhuri wa hakikisho kwamba wewe ni mtoto wa Mungu.

*Siku ya 15*

*Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu. Mimi nalikuja ili wawe na uzima,*
*kisha wawe nao tele.*

Yohana 10:10

SIKU YA 15

# Uzima na Kifo Wakati wa Krismasi

Nilipokuwa karibu na kuanza kutayarisha haya masomo ya kutafakari Krismasi, nilipata habari kwamba Marion Newstrum alikuwa amekufa muda mchache uliopita. Marion na mumewe, Elmer, walikuwa sehemu ya kanisa letu kwa muda mrefu. Walikuwa kanisani kwa muda mrefu kushinda umri wa wengi kanisani humu. Alikuwa na miaka themanini na saba. Walikuwa wameoana kwa miaka sitini na minne.

Nilipozungumza na Elmer na nikamwambia nilitaka awe na nguvu katika Bwana na asikate tamaa ya maisha, alisema, "Kristo amekuwa rafiki wa kweli."

Ninaomba kwamba Wakristo wote wataweza kusema watakapofikia mwisho wa maisha kwamba, "Kristo amekuwa rafiki wa kweli." Kila Majira ya Krismasi huwa ninakumbuka mwaka ambao mama alikufa. Alikatishwa

maisha yake akiwa na miaka hamsini na sita katika ajali ya barabarani kule Israeli. Ilikuwa 16, Disemba 1974. Inashangaza kwamba hayo machungu bado ni halisi kwangu hata leo. Nikifikiria kuhusu janga hili, ninaweza kuangua kilio kirahisi—kwa mfano, nikikumbuka kwamba wanangu wa kiume hawakuwahi kumjua. Tulimzika siku iliyofuata Krismasi. Ilikuwa Krismasi ya thamani iliyoje!

Wengi wenu watahisi hasara yenu Krismasi hii kwa uchungu zaidi kuliko awali. Usiizuie. Iache ije. Ihisi tu. Upendo ni wa nini, kama si kuvumisha mapenzi yetu—katika uzima na katika kifo? Lakini, usiwe na uchungu. Kuwa na uchungu ni kujiharibu mwenyewe kunakoweza kukuletea balaa.

Yesu alikuja Krismasi ili tuwe na uzima wa milele. "Nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele" (Yohana 10:10). Elmer na Marion walikuwa wamejadiliana kuhusu mahali ambapo wangeishi miaka yao ya mwisho. Elmer akasema, "Mimi na Marion tulikubaliana kwamba nyumba yetu ya mwisho itakuwa kuwa na Bwana."

Je, wewe unahisi hamu ya kwenda nyumbani? Nina familia ambayo inakuja nyumbani kwa likizo. Ninasikia furaha. Nafikiri sababu kuu ya kusikia furaha ni kwamba mimi na wao tumejaliwa katika kina cha utu wetu kuwa na kurudi nyumbani – yaani kwenda mbinguni wakati wa

mwisho. Kurudi nyumbani kwingine kwote ni kionjo tu. Na vionjo ni vizuri.

Isipokuwa vinapokuwa mbadala. Usiache mambo yote matamu ya haya majira yawe mbadala ya utamu wa mwisho, ulio mkuu na unaotosheleza vyote. Acha kila hasara na kila furaha iletee mioyo yenu hamu ya kwenda mbinguni. Krismasi hii ndiyo Krismasi, si vingine: *Nalikuja ili wawe na uzima?* Marion Newstrum, Ruth Piper, na mimi na wewe—ili tuwe na uzima, sasa na hata milele.

Ifanye *sasa* yako iwe tajiri zaidi na ya ndani zaidi Krismasi hii kwa kunywa kutoka katika chemchemi ya *milele*. Iko karibu sana.

*Siku ya 16*

*Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina, ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi, na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwama, kwa utukufu wa Mungu Baba.*

Wafilipi 2:9–11

SIKU YA 16

# Unyonge wa Mungu Uliostawi Kabisa

Krismasi ndiyo iliyokuwa mwanzo wa kudhihirisha unyonge wa Mungu uliostawi kabisa. Siku zote Mungu amekuwa akionyesha uwezo wake kupitia kwa ushindi wa wazi. Atapiga hatua moja kurudi nyuma kiustadi ili aweze kuadhimisha ushindi mkuu kwa kishindo.

Katika Agano la Kale, Yusufu, mmoja kati ya wana kumi na wawili wa Yakobo, aliahidiwa utukufu na uwezo katika ndoto yake. (Mwanzo 37:5–11). Lakini ili aweze kupata huo ushindi ilimbidi awe mtumwa kule Misri. Na licha ya hilo, wakati hali zake zilipokuwa bora kwa sababu ya uaminifu wake, alifanywa mfungwa: mtu mbaya zaidi ya mtumwa.

Lakini hayo yote yalipangwa—yalipangwa na Mungu kwa wema wake na kwa wema wa familia yake, na hatimaye kwa wema wa ulimwengu mzima! Kwa maana

kule gerezani alikutana na mtunza vileo wa Farao, ambaye hatimaye alimleta kwa Farao, na Farao akamweka juu ya Misri. Na hatimaye ndoto yake ikatimia. Ndugu zake waliinama mbele yake, na akawaokoa wasife kwa pnjaa. Hii si njia ambayo ilionekana kumpeleka katika utukufu!

Lakini hiyo ndiyo njia ya Mungu—hata kwa Mwanawe. Alijivua utukufumwenyewe akachukua nafsi ya mtumwa. Hata namna mbaya zaidi ya mtumwa—mfungwa—na akauawa. Lakini kama Yusufu, alihifadhi uaminifu wake, "Kwa hivyo Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina, ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe" (Wafilipi 2:9–10).

Hii ndiyo njia ya Mungu kwetu sisi pia. Tumeahidiwa utukufu—*ikiwa* tutateseka pamoja naye kama isemavyo katika Warumi 8:17. Njia ya kupanda juu iko chini. Njia ya kusonga mbele inaelekeza nyuma. Njia ya kupata mafanikio inapitia vipingamizi chungu nzima zinazoletwa na Mungu. Siku nyingi unaonekana na kuhisiwa kuwa umeshindwa.

Lakini kama Yusufu na Yesu wanatufundisha chochote Krismasi hii, ni hili: Yale ambayo Shetani na wenye dhambi walikusudia mabaya, "Mungu aliyakusudia kuwa mema..." (Mwanzo 50:20).

Enyi watakatifu wenye hofu vaeni ujasiri mpya
Mawingu yawatishayo sana
Yamejaa rehema yatayeyuka
Na baraka kumimina mwenu vichwani.[4]

4 William Cowper, "God Moves in a Mysterious Way," 1773

*Siku ya 17*

*Angalia, siku zinakuja, asema Bwana, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda.*

Yeremia 31:31

SIKU YA 17

# Wokovu Mkuu Zaidi Unaoweza Kufikirika

Mungu ni mwenye haki na mtakatifu amejitenga na wenye dhambi kama sisi.

Hili ndilo tatizo letu kuu wakati wa Krismasi—na majira mengine yoyote. Tutawezaje kupatana na Mungu mwenye haki na aliye mtakatifu?

Hata hivyo, Mungu ana huruma na ameahidi katika Yeremia 31 (miaka mia tano kabla ya Kristo) kwamba siku moja angefanya jambo jipya. Angefanya uhalisi wa Masihi uchukue nafasi ya mifano. Kwamba angeingia maishani mwetu kwa uwezo na kuandika upendo wake mioyoni mwetu ili tusilazimishwe kumpenda kutoka nje bali tumpende kutoka ndani; kumpenda yeye, kumwamini na kumfuata.

Huo utakuwa wokovu mkuu zaidi unaoweza kufikirika—kama Mungu atatupatia uhalisi mkuu zaidi

hapa ulimwenguni. Ili tufurahie wokovu wetu na kisha aingie ndani yetu ili tujue uhalisi huo kwa njia ambayo itaweza kusababisha uhuru mkuu zaidi na furaha kuu zaidi iwezekanayo. Hiyo itakuwa ni zawadi ya Krismasi inayostahili kuimbiwa.

Kwa kweli hivyo ndivyo alivyoahidi katika Agano Jipya. Lakini kulikuwa na kikwazo kikubwa. Dhambi yetu. Kutengwa kwetu na Mungu kwa sababu ya uovu wetu.

Ni kwa jinsi gani Mungu mtakatifu na mwenye haki anatutendea sisi wenye dhambi wema mwingi sana kwa kutupatia uhalisi mkuu zaidi hapa ulimwenguni (Mwanawe) ili tufurahie zaidi iwezekanayo?

Jibu ni kwamba Mungu aliweka dhambi zetu juu ya Mwanawe na akazihukumu hapo, ili aweze kuzitoa akilini mwake na atushughulikie sisi kwa rehema na yeye abaki kuwa mwenye haki na mtakatifu kwa wakati mmoja. Waebrania 9:28 inasema Kristo "alitolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi."

Kristo alizichukua dhambi zetu katika mwili wake alipokufa (1 Petro 2:24). Alichukua hukumu yetu (Warumi 8:3). Alifuta hatia yetu (Warumi 8:1). Hilo linamaanisha kwamba dhambi zetu hazipo tena. (Matendo 10:43). Hazipo tena katika akili ya Mungu kama sababu ya sisi kuhukumiwa. Kwa maana hiyo, yeye "huzisahau" (tazama Yeremia 31:34). Zimemezwa katika kifo cha Kristo.

Hilo lina maana kwamba Mungu sasa yuko huru kutumiminia utimilivu wa ahadi zake zote kuu za agano jipya zisizoweza kuelezeka. Atatupatia Kristo, uhalisi mkuu zaidi hapa ulimwenguni ili tufurahie. Na anaandika nia yake mwenyewe—moyo wake mwenyewe—juu ya mioyo yetu ili tuweze kumpenda Kristo na tumwamini Kristo na tumfuate Kristo kutoka ndani hadi nje, kwa uhuruna furaha.

*Siku ya 18*

*Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni.*

Yohana 17:18

SIKU YA 18

# Krismasi kama Kielelezo cha Uinjilisti

Krismasi ni kielelezo cha uinjilisti. Uinjilisti ni kioo cha Krismasi.

Kwa mfano, hatari. Kristo alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Hata wewe hutapokewa. Walimpangia hila. Hata wewe utapangiwa. Hakuwa na nyumba ya kudumu. Hata wewe pia huna nyumba ya kudumu. Walimtungia mashtaka ya uongo. Hata wewe watakufanyia hivyo. Walimpiga na kumdhihaki. Hata wewe watakufanyia hivyo. Alikufa baada ya miaka mitatu ya huduma. Hata wewe pia.

Lakini kuna hatari mbaya zaidi kuliko hizi zote, ambayo Yesu *aliiepuka*. Hata wewe pia utaiepuka!

Katika miaka ya katikati ya karne ya kumi na sita mmishenari Francis Xavier (1506–1552) alimwandikia Perez, Kasisi wa Malaka (leo ni sehemu ya Malaysia)

kuhusu hatari za misheni yake kule Uchina. Alisema, "Hatari kubwa kuliko zote ni ile ya kupoteza uaminifu na uhakika katika rehema za Mungu... Kutomwamini kutakuwa jambo la kutisha zaidi kuliko uovu wowote wa kimwili ambao maadui wote wa Mungu wakikusanywa pamoja wanaweza kutufanyia. Kwa maana bila ruhusa ya Mungu si mashetani wala mawakala wao wa kibinadamu wanaweza kutuzuia hata kwa kiwango kidogo zaidi."[5]

Hatari kubwa zaidi ambayo mmishenari anaweza kukabiliana nayo si kifo bali ni kutoamini rehema za Mungu. Kama hatari hiyo itaepukwa, basi hatari nyingine zote hupoteza nguvu.

Hatimaye Mungu huufanya kila upanga kuwa fimbo ya utawala mikononi mwetu. Kama J. W. Alexander asemavyo, "Kila tukio la kazi ya sasa linapaswa kulipwa kwa ukarimu na utukufu wa mamilioni ya miaka."[6] Kristo aliepuka hatari hii—hatari ya kutomwamini Mungu. Mungu alimwadhimisha mno. Kama yeye, hata wewe pia.

Kumbuka katika haya majira ya kuja kwa Kristo kwamba Krismasi ni mfano wa misheni. *Kama nilivyo,*

---

5 Kutoka kwa "A Letter to Father Perez," katika Classics of Christian Missions, ed. Francis M. DuBose (Nashville, TN: Broadman Press, 1979), 221f.

6 J. W. Alexander, Thoughts on Preaching: Classic Contributions to Homiletics (Edinburgh: Banner of Truth, 1975), 108.

*ndivyo ulivyo.* Na kwamba maana ya misheni ni hatari. Na hatari kubwa zaidi ni kutoamini rehema za Mungu. Ukiingiwa na hili umepoteza kila kitu. Ukiwa mshindi kwa hili hakuna linaloweza kukudhuru kwa mamilioni ya miaka ijayo.

*Siku ya 19*

*Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa.*

Waebrania 2:14–15

SIKU YA 19

# Krismasi ni ya Kukuweka Huru

Yesu alifanyika mwanadamu kwa sababu kulitakiwa kifo cha mwanadamu aliyekuwa zaidi ya mwanadamu. Kufanywa mwili kulikuwa Mungu alijifungia mwenyewe katika hukumu ya kifo. Kristo hakujihatarisha kufa. Alichagua kufa. Alikubali. Hiyo ndiyo sababu dhahiri iliyomfanya aje: "sio kutumikiwa bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Marko10:45).

Si ajabu Shetani alijaribu kumgeuza Yesu asiende msalabani—kule nyikani (Mathayo 4:1–11) na katika maneno ya Petro (Mathayo 16:21–23)! Msalaba ulinuia kuangamizwa kwa Shetani. Yesu alimwangamiza namna gani?

Waebrania 2:14 inasema kwamba Shetani ana "nguvu ya mauti." Hilo lina maana kwamba Shetani ana uwezo kufanya mauti iogofye. "Nguvu za mauti" ni nguvu zinazowashika wanadamu katika utumwa kwa kupitia hofu

ya mauti. Ni nguvu ya kuwaweka watu katika dhambi ili mauti ije kama kitu cha kutisha.

Lakini Yesu alimpokonya Shetani hizo nguvu. Akampokonya silaha. Akatengeneza dirii ya haki kwa ajili yetu ambayo inatufanya tuwe na kinga dhidi ya hukumu ya ibilisi. Alifanya hivi namna gani? Kwa kifo chake, Yesu alifuta dhambi zetu zote. Mtu asiyekuwa na dhambi hawezi kuhukumiwa na Shetani. Tukiwa tumesamehewa, hatimaye hatuwezi kuharibiwa. Mpango wa Shetani ulikuwa kuharibu sheria ya Mungu kwa kuwahukumu wafuasi wa Mungu katika mahakama ya Mungu mwenyewe. Lakini sasa, katika Kristo, hakuna hukumu. Uhaini wa Shetani umekomeshwa. Udanganyifu wake wa ulimwengu wote umekwamishwa. "Tunaweza kuvumiliaghadhabu yake, kwani, tazama, maangamizi yake ni hakika."[7] Msalaba umemchoma. Na muda si muda ataangamia. Krismasi ni kwa ajili ya uhuru—uhuru kutokana na hofu ya mauti. Yesu alichukua asili yetu kule Bethlehemu ili afe kifo chetu kule Yerusalemu—ili tusiwe na hofu katika maisha yetu leo. Naam, bila hofu, kwa sababu kama tishio kubwa la furaha yetu limeenda, basi kwa nini tuwe na wasiwasi juu ya haya madogo? Tunawezaje kusema (kwa kweli!), "Siogopi kufa lakini naogopa kupoteza kazi yangu"? La! La! Waza!

---

7 Martin Luther, "A Mighty Fortress Is Our God," 1527–1529.

Kama kifo (Nimesema, kifo!—moyo haupigi, uko baridi, umeenda!) si kitu cha kuogopewa tena, basi sisi tuko huru, huru kweli kweli. Tuko huru kuingia katika hatari yoyote chini ya jua kwa ajili ya Kristo na kwa ajili ya upendo. Hakuna tena kufanywa watumwa wa wasiwasi.

Kama Mwana amekuweka huru, basi utakuwa huru kweli kweli!

*Siku ya 20*

*Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi.*

1 Yohana 3:8

SIKU YA 20

# Umoja wa Krismasi

Kiwanda cha Shetani hutoa mamilioni ya dhambi kila siku. Huzipakia katika ndege kubwa za mizigo na kuzipeleka mbinguni na kuzitandaza mbele ya Mungu na kucheka sana sana.

Watu wengine wanafanya kazi wakati wote katika hicho kiwanda. Wengine wameacha kazi zao hapo na hujirudisha mara kwa mara wenyewe mahala hapo.

Kila dakika ya kazi katika hiyo karakana humfanya Mungu adhihakiwe na Shetani. Dhambi ni kazi ya Shetani kwa sababu yeye huchukia nuru na uzuri na usafi na utukufu wa Mungu. Hakuna jambo linalompendeza sana kuliko viumbe wanapokosa kumwamini na kumwasi Muumba wao.

Krismasi ni habari njema kwa mwanadamu na habari njema kwa Mungu.

"Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe

wenye dhambi " (1 Timotheo 1:15). Hiyo ni habari njema kwetu.

"Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi" (1 Yohana 3:8). Hiyo pia ni habari njema kwa Mungu.

Krismasi ni habari njema kwa Mungu kwa sababu Yesu amekuja kuongoza mgomo katika karakana ya Shetani ya kutengeneza dhambi. Ameingia ndani ya karakana hiyo, akawahimiza waumini wawe na umoja, na wakaanza kutoka kwa wingi.

Krismasi ni mwito wa kufanya mgomo katika karakana ya uundaji wa dhambi. Hakuna kujadiliana na wasimamizi wa hiki kiwanda cha hila. Hakuna kuelewana bei. Kwa nia moja, kupinga bidhaa kwa msimamo thabiti. Hatutashiriki tena katika utengenezaji wake.

Umoja wa Krismasi unalenga kuangusha ndege za mizigo. Hautatumia nguvu wala mabavu, lakini kwa kujitoa kwa ukweli bila kukoma kutafunua hali zinazoharibu maisha zitokazo katika kiwanda cha ibilisi.

Umoja wa Krismasi hautakata tamaa mpaka uhakikishe kiwanda hicho kimefungwa kabisa.

Wakati dhambi itakapokuwa imeharibiwa, jina la Mungu litakuwa limetolewa kabisa katika hatia. Hakuna mtu atakayecheka tena. Kama unataka kumpa Mungu zawadi hii Krismasi, toka katika karakana ya dhambi na

usirudi tena. Chukua nafasi yako katika mpaka wa upendo. Jiunge na umoja wa Krismasi mpaka jina kuu la Mungu liondolewe hatia, na asimame kwa utukufu katikati ya sifa kuu za wenye haki.

*Siku ya 21*

*Basi Pilato akamwambia, "Wewe u mfalme basi?" Yesu akajibu, "Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwakwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni—ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu."*

Yohana 18:37

SIKU YA 21

# Kuzaliwa kwa Mwanzilishi wa Nyakati

Yohana 18:37 ni maandiko makuu ya Krismasi hata ingawa inatoka katika mwisho kabisa wa maisha ya Yesu duniani, si mwanzo.

Tambua kwamba Yesu hasemi tu kwamba alizaliwa peke yake, lakini kwamba "[alikuja] ulimwenguni." Upekee wa kuzaliwa kwake ni kwamba hakuanza kuishi wakati wa kuzaliwa kwake. Alikuwapo kabla ya kuzaliwa katika hori. Utu, hulka, haiba ya Yesu wa Nazareti vilikuwako kabla huyo mwanamume Yesu wa Nazareti kuzaliwa.

Neno la kitheologia la kuieleza hii siri si *uumbaji*, bali *kufanyika kuwa mwanadamu.* Yesu alikuwako kabla yeye kuzaliwa kama mwanadamu – alikuwa kama nafsi bila mwili. Kuzaliwa kwake hakukuwa kuwako kwa mtu mpya, bali kuja ulimwenguni kwa mtu asiyekuwa na mwisho.

Mika 5:2 inaisema namna hii, miaka mia saba kabla Yesu kuzaliwa:

> Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda, kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli, ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele.

Ajabu ya kuzaliwa kwa Yesu si tu kwamba alizaliwa na bikira. Huo muujiza ulikusudiwa na Mungu ili uwe ushahidi wa muujiza mkuu zaidi, yaani kwamba huyo mtoto aliyezaliwa Krismasi alikuwa mtu aliyekuwako "tangu zamani za kale, tangu milele."

Na kwa hivyo, kuzaliwa kwake kulikuwa na lengo. Kabla yeyekuzaliwa, aliwaza kuhusu kuzaliwa. Pamoja na Baba yake kulikuwa na mpango. Na sehemu ya huo mpango mkubwa aliisema katika masaa ya mwisho ya uhai wake hapa duniani: "Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni—ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu" (Yohana 18:37).

Alikuwa kweli ya milele. Alisema ukweli pekee yake. Yeye aliuonyesha ukweli mkuu wa upendo. Na anakusanya

katika familia yake ya milele wale wote waliozaliwa katika kweli. Huu ndio uliokuwa mpango tangu milele.

*Siku ya 22*

*Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*

Yohana 20:30-31

SIKU YA 22

# Ndiposa Uweze Kuamini

Ninahisi kwamba sisi ambao tumekua tukiwa kanisani na ambao tunaweza kukariri mafundisho makuu ya imani yetu na kuinena kwa ufasaha Imani ya Mitume tuna jukumu. Lazima tuchukue hatua itusaidie kuhisi hiyo hofu kwa mara nyingine tena, uoga, mshangao, ajabu ya Mwana wa Mungu. Yule aliyezaliwa na Baba kutoka milele yote, akionyesha utukufu wote wa Mungu, akiwa mfano hasa wa utu wake. Kupitia yeye vitu vyote viliumbwa. Anashikilia ulimwengu kwa neno la uwezo wake.

Unaweza kusoma kila hadithi iliyowahi kuandikwa, kila tamthilia ya ajabu ya kusisimua, kila hadithi ya pepo, na kamwe hutapata chochote cha kushangaza, cha ajabu, cha kuogofya na kutamausha kama hadithi ya Mwana wa Mungu kufanyika kuwa mwanadamu.

Sisi ni kama watu waliokufa fofofo! Sisi ni sugu sana na hatuna hisia kabisa kwa utukufu wako na hadithi yako, Ee

Mungu.! Ni mara ngapi nimelazimika kutubu na kusema, "Mungu, samahani kwamba hadithi ambazo wanadamu wametunga huchochea mihemko yangu, hofu yangu na kushangaa nakuvutiwa na furaha, zaidi ya hadithi yako ya kweli."

Pengine michezo ya kuigiza na kusisimua kuhusu mambo ya angani ya siku zetu inaweza angalau kutufanyia uzuri huu: inaweza kutufanya tunyenyekee na kutubu, kwa kutuonyesha kuwa kwa kweli tunawezakuona ajabu na hofu na tukashangaa. Haya yote ni nadra sana sisi kuyahisi wakati tunapotafakari Mungu wa milele na utukufu wa Kristo wa kilimwengu na kukutana nayo kikweli kweli katika Yesu wa Nazareti.

Yesu aliposema, "Kwa ajili ya haya nalikuja ulimwenguni" (Yohana 18:37), alisema kitu cha kutamausha na kuogofya kisichokuwa cha kawaida, na cha kushtua kama kauli yoyote ya kufikirika ya kisayansi uliyowahi kusoma.

Ninaomba sana Roho wa Mungu aje kwa nguvu juu yangu na juu yako, Roho Mtakatifu aingie kwa nguvu ndani ya uzoefu wangu kwa njia ya kuogofya, ili aniamshe niuone uhalisi wa Mungu usioweza kufikirika.

Siku moja hivi karibuni radi itaijaza anga kuanzia mawio ya jua hadi machweo yake, na kule mawinguni kutatokea Mwana wa Adamu na malaika wake wakuu katika miale ya moto. Na tutamwona waziwazi. Na tutatetemeka, kuwe

kutokana na kutishika au kusisimka tu, na tutajiuliza jinsi tulivyoishi kwa muda mrefu sana na Kristo anayependa maisha ya familia, asiyemdhuru yeyote.

Mambo haya yameandikwa—Biblia nzima imeandikwa—ili tuweze kuamini, ili tuweze kushtuliwa na kuamka na kushangaa, kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu aliyekuja ulimwenguni.

*Siku ya 23*

*Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake. Wala si hivyo tu, ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye sasa tumeupokea huo upatanisho.*

Warumi 5:10–11

SIKU YA 23

# Zawadi ya Ajabu ya Mungu

Kiutendaji, tunawezaje kupatanishwa na Mungu na kupata furaha katika muungano wetu na yeye? Tunafanya hivyo kupitia kwa Yesu Kristo. Hii ina maana kwamba tunachora picha ya Yesu katika Biblia. Yaani, kazi na maneno ya Yesu yanavyoonyeshwa katika Agano Jipya—mambo ya kimsingi yaliyomo katika furaha yetu juu ya Mungu. Kufurahi katika muungano wetu na Mungu bila yaliyomo katika Kristo hakumpi heshima Kristo. Na mahali ambapo Kristo haheshimiwi Mungu pia haheshimiwi.

Katika 2 Wakorintho 4:4–6 Paulo anaeleza kuokolewa katika njia mbili. Katika kifungu cha 4 anasema ni kuona "utukufu wa Kristo, ambaye ndiye mfano wa Mungu." Na katika kifungu cha 6 anasema ni kuona "utukufu wa Mungu katika sura ya Yesu Kristo." Katika njia yoyote kati ya hizo unaona hilo wazo. Tunaye Kristo, mfano wa Mungu, na tunaye Mungu katika sura ya Kristo.

Kufurahi katika muungano wetu na Mungu, tunafurahia katika kile tunachoona na kujua kuhusu Mungu katika picha ya Yesu Kristo. Na furaha hii inafikia ukamilifu wake wakati upendo wa Mungu unapomiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu, kama Warumi 5:5 inavyosema. Na hiyo furaha tamu, ya upendo wa Mungu inayotolewa na Roho inaletwa kwetu tunapotafakari kuhusu uhalisi wa kihistoria wa kifungu cha 6: "Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu."

Kwa hivyo, wazo la Krismasi ni hili. Mungu hakununua tu upatanisho wetu pekee kupitia kwa kifo cha Bwana Yesu Kristo (Warumi 5:10), na Mungu hakutuwezesha sisi kupokea huo upatanisho kupitia kwa Bwana Yesu Kristo peke yake, lakini hata sasa tunamfurahia Mungu mwenyewe, kwa Roho, kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo (Warumi 5:11).

*Yesu alinunua upatanisho wetu.* Yesu alituwezesha kupokea upatanisho na kufungua hicho kipawa. Yesu mwenyewe humulika hiyo zawadi isiyoelezeka kama yeye mwenyewe—Mungu katika mwili—na huchochea furaha yetu yote katika muungano wetu na Mungu.

Mwangalie Yesu Krismasi hii. Pokea huo upatanisho aliounununua. Usiweke hiyo zawadi juu ya rafu bila kuifungua. Na unapoifungua, kumbuka Mungu mwenyewe ndiye hiyo

zawadi ya upatanisho na Mungu. Furahi katika kuungana na yeye. Mchukue kama raha yako. Mjue yeye kama hazina yako.

*Siku ya 24*

*Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyo na haki; atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisil.*

1 Yohana 3:7–8 (SUV)

SIKU YA 24

# Malengo Mawili ya Krismasi

1 Yohana 3:8 anaposema, "Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi," Ni "kazi za Ibilisi" zipi zilizokuwa akilini mwake? Jibu liko wazi kutokana na muktadha.

Kwanza, 1 Yohana 3:5 ina usambamba ulio wazi: "Nanyi mnajua ya kuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi." Msemo kwamba *yeye alidhihirishwa* uko katika kifungu cha 5 na kifungu cha 8. Kwa hivyo, inaelekea kuwa "kazi za ibilisi" ambazo Yesu alikuja kuharibu ni dhambi. Sehemu ya kwanza ya kifungu cha 8 inafanya hili kuwa ukweli wa hakika: "Kila *atendaye dhambi* ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo."

Suala lililo katika huu muktadha ni *kutenda dhambi*, si magonjwa au magari yaliyoharibika au ratiba zilizovurugika. Yesu alikuja ulimwenguni *atuwezeshe kuacha dhambi.*

Tunaona hili kwa uwazi zaidi tukiweka ukweli huu pamoja na ukweli wa 1 Yohana 2:1: "Watoto wangu

wadogo, nawaandikia haya ilii kwamba msitende dhambi." Hili ni moja wapo ya malengo makuu ya Krismasi—moja wapo ya malengo makuu ya Yesu kuzaliwa kuwa mwanadamu (1 Yohana 3:8).

Lakini kuna lengo lingine ambalo Yohana analiongeza katika 1 Yohana 2:1–2: "Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki. Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote."

Sasa tazama hili linamaanisha nini: linamaanisha kwamba Yesu alidhihirishwa ulimwenguni kwa sababu mbili. Alikuja ili tusiweze kuendelea kutenda dhambi—yaani, alikuja kuharibu kazi za ibilisi (1 Yohana 3:8); na alikuja ili kuwe na kipatanisho kwa dhambi zetu kama tutatenda dhambi. Alikuja ili awe sadaka mbadala inayoondoa ghadhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi zetu. Matokeo ya lengo hili la pili si kulishinda lengo la kwanza. Lengo la msamaha si kuruhusu dhambi. Lengo la kifo cha Kristo kwa ajili ya dhambi zetu si kwamba tuache vita vyetu dhidi ya dhambi. Matokeo ya haya malengo mawili ya Krismasi, badala yake, ni kwamba malipo yaliyotolewa mara moja kwa ajili ya dhambi zetu zote ni uhuru na uwezo wa kutuwezesha sisi tupigane na dhambi si kama washikiliaji mno wa sheria, tukifanyia kazi wokovu wetu, na bila kuogopa kwamba tunaweza kuupoteza

wokovu wetu, bali kama washindi ambao tunajiingiza katika vita dhidi ya dhambi. Tunafanya hivi huku tuna uhakika na furaha, hata kama itatugharimu maisha yetu.

*Siku ya 25*

*Watoto wangu wadogo,*
*nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi.*
*Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki. naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote... Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye. Atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyo na haki. Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi.*

1 Yohana 2:1–2; 3:7–8

SIKU YA 25

# Zawadi Tatu za Krismasi

Hebu tafakari pamoja nami hali hii ya ajabu. Kama Mwana wa Mungu alikuja ili akusaidie kuacha dhambi—ili aziharibu kazi za ibilisi—na kama pia alikuja ili afe ndiposa wewe unapofanya dhambi, kuna kipatanisho, kuondolewa kwa ghadhabu ya Mungu, basi hili linamaanisha nini kwa ajili ya kuishi maisha yako?

Mambo matatu. Na ni mazuri sana kuwa nayo. Ninakupa wewe mambo hayo kwa kifupi kama zawadi za Krismasi.

## *Zawadi ya 1: Lengo Lililo Wazi la Maisha*

Maana ya kwanza ni kwamba una lengo lililo wazi la maisha. Ukisema kwa kukanusha, ni hivi tu: usitende dhambi—usifanye kitu kinachomvunjia heshima Mungu. "Nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi" (1 Yohana 2:1). "Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi" (1 Yohana 3:8).

Ukiuliza, "Je, unaweza kusema hayo kwa njia chanya, badala ya njia hasi?" "Ndio, yote yanajumulishwa katika" 1 Yohana 3:23.

Ni muhtasari wa yale yote ambayo barua ya Yohana inayataka. Tambua hali ya umoja ya "amri"—"Na hii ndiyo *amri* yake, kwamba tuliamini jina la Mwana wake Yesu Kristo, na kupendana sisi kwa sisi, kama alivyotupa amri." Haya mambo mawili yana uhusiano wa karibu sana kwa Yohana hivi kwamba anayaita amri moja: mwamini Yesu na uwapende wengine. Hilo ndilo lengo lako. Hiyo ndiyo jumla ya maisha ya Mkristo. Kumwamini Yesu na kuwapenda watu kwa njia ambayo Yesu na mitume wake walitufundisha kupenda. Mwamini Yesu, uwapende watu. Hiyo ndiyo zawadi ya kwanza, lengo la kuishi.

## *Zawadi ya 2: Tumaini Kushindwa Kwetu Kutasamehewa*

Maana ya pili ya ukweli wenye sehemu mbili ambao Kristo alikuja kuharibu utenda dhambi wetu na atusamehe dhambi zetu ni hii: tuendelee kushinda dhambi zetu wakati tunapokuwa na tumaini kwamba kushindwa kwetu kutasamehewa. Kama wewe huna tumaini kwamba Mungu atasamehe kushindwa kwako, unapoanzakupigana na dhambi, unavunjika moyo.

Wengi wenu mnatafakari mabadiliko fulani katika mwaka mpya kwa sababu umeanguka katika michafuko ya dhambi na unataka kutoka. Unataka mitindo mipya ya kula. Mitindo mipya ya matumbuizo. Mitindo mipya ya kutoa. Mitindo mipya ya kuhusiana na mwenzako. Mitindo mipya ya ibada za kifamilia. Mitindo mipya ya kulala na kufanya mazoezi.

Mitindo mipya ya ujasiri katika kuwashuhudia watu. Lakini unang'ang'ana, ukijiuliza kama ina maana yoyote. Hapa kuna zawadi yako ya pili ya Krismasi: Kristo hakuja kuharibu tu kazi za ibilisi, kutenda dhambi kwetu; pia alikuja ili awe wakili wetu kwa sababu ya matukio ya kushindwa katika vita vyetu.

Kwa hivyo, ninawasihi, hebu acheni ukweli kwamba kushindwa hakutakuwa na uamuzi wa mwisho, uwape tumaini la kupigana. Lakini chungeni! Mkiigeuza neema ya Mungu na kuwa liseni, na mseme, "Kama ninaweza kushindwa, na sitapoteza chochote, basi kwa nini nijisumbue kupigana na dhambi?"Ukisema hivyo, na umaanishe, na uendelee kulifanyia kazi, yamkini wewe hujazaliwa mara ya pili na unapaswa kutetemeka. Lakini hapo sipo wengi wenu walipo. Wengi wenu wanataka kupigana na mitindo ya dhambi maishani mwenu. Na kile ambacho Mungu anasema nanyi ni hiki: Kristo anafunika

kushindwa kwenu. Acheni kufunika huko kumpe tumaini la kupigana. "Nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi, Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo."

### *Zawadi ya 3: Kristo Atatusaidia*

Hatimaye, maana ya tatu ya ukweli wenye sehemu mbili ambao Kristo alikuja kuharibu utenda dhambi wetu na atusamehe dhambi zetu ni hii: Kwa kweli Kristo atatusaidia katika vita vyetu. Kwa kweli atakusaidia. Yeye yuko upande wako. Hakuja kuharibu dhambi kwa sababu dhambi inafurahisha. Alikuja kuharibu dhambi kwa sababu dhambi inaua. Ni kazi ya uongo wa ibilisi, na itatuharibu kama hatutapigana nayo. Alikuja kutusaidia, sio kutuumiza.

Kwa hivyo, hapa kuna zawadi yako ya tatu ya Krismasi: Kristo atakusaidia ushinde dhambi ndani yako. Yohana wa Kwanza 4:4 inasema, "yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Yesu yuko hai, Yesu ni mwenye nguvu zote, Yesu anaishi ndani yetu kwa imani. Yesu yuko upande wetu, si kinyume chetu. Atakusaidia katika vita vyako na dhambi katika huu mwaka mpya. Mwamini yeye.

*Hitimisho*

HITIMISHO

# Maandiko yangu ya Krismasi Niyapendayo Zaidi

Maandiko ya Krismasi ninayopenda zaidi yanatia unyenyekevu katika moyo wangu. Kwa hivyo, hii Krismasi ninashangazwa na unyenyekevu wa Yesu na kutaka unyenyekevu zaidi kwa ajili yangu mimi. Nitakinukuu hicho kifungu hivi punde.

Lakini kwanza kuna matatizo mawili. Tim Keller anatusaidia kuona tatizo mojawapo anaposema, "Unyenyekevu una haya sana. Ukianza kuuzungumzia, unaondoka." Kwa hivyo kutafakari juu ya unyenyekevu (kama huu) kunaonekana hakutafaulu. Lakini hata watu wenye haya wakati mwingine huchungulia wakifanyiwa wema. Tatizo lingine ni kwamba Yesu hakuwa mnyenyekevu kwa sababu zile zile zinazotufanya sisi tuwe (au tupaswe kuwa) wanyenyekevu. Kwa hivyo, kuangalia unyenyekevu wa Yesu wa Krismasi kutatusaidia namna gani?

Unyenyekevu wetu, kama upo wowote, msingi wake ni kwamba: sisi tuna upungufu, tunaweza kukosa, na ni watenda dhambi. Lakini Mwana wa milele wa Mungu hakuwa na upungufu. Hakuwa na makosa. Na hakuwa na dhambi. Kwa hiyo, chanzo cha unyenyekevu wetu, si sawa na chanzo cha unyenyekevu wa Yesu.

Kifungu cha Krismasi ninachokipenda zaidi ndicho hiki. Utafute unyenyekevu wa Yesu:

> Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna
> ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na
> Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho,bali
> alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna
> ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu.
> tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu,
> *alijinyenyekeza* akawa mtii hata mauti, naam, mauti
> ya msalaba. (Wafilipi 2:6–8)

Kinachofasili unyenyekevu wa Yesu ni ukweli kwamba sana sana ni kitendo alichokifanya kwa kufahamu. Kujitia mwenyewe katika wajibu duni wa kuwa mtumwa kwa wema wa watu wengine. Unyenyekevu wake unafasiliwa na virai kama hivi:

> "Alijifanya kuwa hana utukufu [wa haki zake za kiungu za kutoweza kutukanwa na kuteseka]."
> "Akachukua namna ya mtumwa."
> "Akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba."

Kwa hivyo, unyenyekevu wa Yesu haukuwa tabia ya moyo ya kuwa na upungufu, au kuweza kukosa au kuwa mtenda dhambi. Ulikuwa ni moyo wa ukamilifu usiokuwa na mipaka na ukweli usioweza kukosea na uhuru kutoka kwa dhambi zote, ambazo kwa sababu iyo hiyo hakuwa na haja ya kutumikiwa. Alikuwa huru na alikuwa amejaa ili aweze kububujika na kutumika.

Kifungu kingine cha Krismasi kinachosema hivi ni Marko 10:45: "Mwana wa Adamu *naye hakuja kutumikiwa* bali *kutumika*, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" Unyenyekevu wa Yesu haukuwa na maana ya kujiasi mwenyewe, lakini maana ya ujazo ndani yake mwenyewe uliowekwa kwa manufaa ya wengine kwa ajili ya wema wao. Ulikuwa wa kujishusha kwa hiari yake mwenyewe ili afanye kimo cha utukufu wake kipatikane ili wenye dhambi wapate kukifurahia.

Yesu huleta uhusiano kati ya hali yake ya chini ya Krismasi na habari njema kwa ajili yetu: "Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu mjifunze kwangu,

kwa kuwa mimi ni *mpole* na *mnyenyekevu wa moyo,* nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi" (Mathayo 11:28–30). Unyenyekevu wake unafanya tuweze kupumzika kutokana na mizigo yetu. Kama hangekuwa mnyenyekevu, hangekuwa "mtiifu hata kwa mauti, naam, mauti ya msalaba." Kama hangekuwa mtiifu kwa kufa kwa ajili yetu, tungekuwa tumesagwa chini ya uzito wa dhambi zetu. Anajinyenyekeza ili achukue hukumu yetu (Warumi 8:3).

Sasa tuna sababu zaidi za kuwa wanyenyekevu kuliko hapo awali. Tuna upungufu, tuna kosa, na tu wenye dhambi na kwa hivyo hatuna sababu ya kujivuna kabisa. Lakini sasa tunaona mambo mengine ya kutufanya tunyenyekee: wokovu wetu si kwa sababu ya kazi yetu, lakini ni kwa sababu ya neema yake. Kwa hivyo, hakuna kujisifu kabisa (Waefeso 2:8–9). Jinsi alivyotimiza huo wokovu wa neema ilikuwa kupitia kwa utiifu wa mauti. Kujitolea, kujinyenyekeza kwa utiifu kama wa mtumwa.

Kwa hivyo, pamoja na kuwa na upungufu, kuweza kukosa, na kuwa wenye dhambi, sasa tuna misukumo mingine miwili mikubwa inayofanya kazi ya kutufanya tunyenyekee: neema ya bure tusiyostahili chini ya baraka zetu zote na kielelezo cha kujikana wenyewe, utumishi wa kujitoa ambao unachukua namna ya mtumwa kwa kupenda.

Kwa hivyo tunaitwa tuungane na Yesu katika huku kujinyenyekeza na kuwa kama watumwa. “Na ye yote atakayejikweza, atadhiliwa; na ye yote atakayejidhili, atakwezwa.” (Mathayo 23:12). “Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu, ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu …” (Wafilipi 2:5). Tuombe kwamba hii “hulka ya kuwa na haya”—iwe sababu kubwa ya wokovu wetu na utumwa wetu. Ujitoe kutoka katika pahali pake pa unyamavu na utupatie mavazi ya unyenyekevu katika haya majira ya Krismasi. “Ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema.” (1 Petro 5:5).

# *Kiambatisho*

KIAMBATISHO

# Mifano ya Agano la Kale na Kuja kwa Kristo

Wazo mojawapo kati ya mawazo makuu ya kitabu cha Waebrania ni kwamba mfumo wa ibada wa Agano la Kale ni kivuli ambacho nafasi yake ilichukuliwa na Kristo. Kwa hivyo Krismasi ni nafasi ya *vivuli/mifano* kuchukuliwa na uhalisi. (Unaweza kuona hili katika Waebrania 8:5, ambapo inasema kwamba makuhani "watumikiao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni.") Angalia mifano sita kama hiyo ambayo inachukuliwa na uhalisia kutokana na kuja kwa Kristo.

### *1. Kivuli cha ukuhani wa Agano la Kale.*

Makuhani wa kale walikuwa wengi, kwa sababu walizuiwa na kifo wasiendelee kutumika, lakini Yesu anashikilia *ukuhani wake milele,* kwa sababu yeye anaendelea milele. (Waebrania 7:23–24)

### *2. Kivuli cha sadaka ya Pasaka.*

Basi, jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya,kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana *Pasaka wetu* yaani *Kristo* amekwisha kutolewa sadaka. (1 Wakorintho 5:7 SUV).

### *3. Kivuli cha hema na hekalu.*

Basi, katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili: Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha ukuu mbinguni, mhudumu wa patakatifu, na wa ile *hema ya kweli*, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu. (Waebrania 8:1–2 SUV)

Yesu akajibu, akawaambia, “Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha.” Basi Wayahudi wakasema, “Hekalu hili lilijengwa katika muda wa miaka arobaini na sita, nawe utalisimamisha katika siku tatu?” Lakini yeye alinena habari za *hekalu la mwili wake*. (Yohana 2:19–21)

### *4. Kivuli cha tohara.*

Kutahiriwa si kitu, na kutotahiriwa si kitu, bali kuzihifadhi amri za Mungu. (1 Wakorintho 7:19 SUV)

### *5. Kivuli cha sheria za chakula.*

Akawaambia, “Hivi hata ninyi hamna akili? Hamfahamu ya kwamba kila kitu kilicho nje ya mtu, kikimwingia, hakiwezi kumtia unajisi, kwa sababu hakimwingii moyoni, ila tumboni tu; kisha chatoka kwenda chooni?” (Kwa kusema hivi *alivitakasa vyakula vyote*...) (Marko 7:18–19 SUV)

### *6. Kivuli cha siku kuu.*

Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya siku kuu au mwandamo wa mwezi, au Sabato—mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali *ukweli halisi ni wa Kristo*. (Wakolosai 2:16–17 SUV).

Maana ya Krismasi ni kwamba mwili ni wa Kristo. Yaani tambiko la kidini ni kama kivuli cha mtu mkuu na wa utukufu. Natukiache hicho kivuli na tumwangalie huyo mtu usoni (2 Wakorintho 4:6). Watoto wadogo, jilindeni nafsi zenu (kidini) na sanamu (1 Yohana 5:21).

desiringGod

Kila mtu anataka kuwa na furaha. Tuvuti yetu ilifunguliwa na kujengwa kwa ajili ya kuwaletea watu furaha. Tunataka watu kila mahali waelewe na wakubali ukweli kwamba Mungu anatukuzwa sana ndani yetu wakati tunapotosheka sana ndani yake. Tumekusanya zaidi ya miaka thelathini ya hotuba na maandishi ya John Piper, pamoja na tafsiri katika zaidi ya lugha arobaini. Pia tunatoa msururu wa zana mpya za maandishi, kanda za kusikiliza, na video ili zikusaidie kupata ukweli, lengo, na kutosheka kusikoisha kamwe. Na zote zinapatikana bila malipo, shukrani kwa ukarimu wa watu ambao wamebarikiwa na huduma.

Kama unataka vitabu zaidi vya furaha ya kweli, au kama unataka kujifunza zaidi kuhusu kazi yetu hapa *Desiring God*, tunakukaribisha ututembelee hapa desiringGod.org.

# Faharasa ya Maandiko


*Mwanzo*
37:5–11 .................. 86
50:20 ...................... 87

*Kumbukumbu la Torati*
10:17 ...................... 57

*Zaburi*
139:23–24 ............. 19

*Mithali*
21:1 ........................ 31

*Isaya*
8:18 ........................ 63
53:10 ...................... 63
60:3 ........................ 44

*Yeremia*
23:29 ...................... 19
31 .......................... 91
31:31 ...................... 90
31:34 ...................... 92

*Mika*
5:2 .......................... 112, 30

*Mathayo*
2:1–2 ...................... 42
2:2 .......................... 46, 47
2:3 .......................... 54, 56
2:4 .......................... 53
2:9 .......................... 47
2:10 ........................ 58
2:10–11 .................. 58
4:1–11 .................... 101
11:28–30 ................ 139
16:21–23 ................ 101
23:12 ...................... 140
24:14 ...................... 49
28:18–19 ................ 43

*Marko*
7:18–19 .................. 144
10:45 ...................... 101, 138

*Luka*
1:16–17 .................. 20
1:43 ........................ 23
1:46–55 .................. 21
1:48 ........................ 23
1:68 ........................ 26
1:68–71 .................. 25, 26
2:1–5 ...................... 29
2:6–7 ...................... 34
2:11 ........................ 18
2:12–14 .................. 38
2:25 ........................ 27
2:34–35 .................. 39
2:38 ........................ 27
9:23 ........................ 36
9:57–58 .................. 36
22:20 ...................... 76

*Yohana*
1:1 ......................... 63
1:3 ......................... 13
1:11–12 ................. 40
1:12 ....................... 12, 63,
2:19–21 ................. 142
3:16 ....................... 63
3:17 ....................... 12
3:19 ....................... 39
4:23 ....................... 49
6:35 ....................... 12
6:44 ....................... 12
6:65 ....................... 12
10:10 ..................... 80, 82
10:11 ................ 12
10:17–18 .......... 12
11:52 ................ 63
14:27 ................ 40
15:20 ................ 36
17:24 ................ 11
17:18 ................ 95
18:37 ................ 117, 112, 111
20:28 ................ 12
20:30–31...........115

*Matendo*
10:43 ................ 92
17:25 ................ 57

*Warumi*
5:5 .................... 122
5:9 .................... 64
5:10 .................. 122
5:10–11 ............ 120
5:11 .................. 122
8:1 .................... 92
8:3 .................... 92, 139
8:17 .................. 87
8:33 .................. 64
15:13 ................ 40

*1 Wakorintho*
5:7 .................... 143
7:19 .................. 143

*2 Wakorintho*
4:4–6 .............. 121
4:6 .................. 144
8:9 .................. 36

*Waefeso*
2:8–9 .............. 139

*Wafilipi*
2:5 .................. 140
2:6–8 .............. 137
2:9–10 ............ 87
2:9–11 ............ 85
4:6–7 .............. 40

*Wakolosai*
2:9 .................. 63
2:16–17 .......... 144

*1 Timotheo*
1:15 ................ 107
4:10 ................ 63

*Waebrania*
2:13 ................ 62
2:14 ................ 101
2:14–15 .......... 62, 100
7:23–24 .......... 142
8:1 .................. 73
8:1–2 .............. 67, 71, 72, 143
8:2 .................. 72
8:5 .................. 71, 72, 142
8:6 .................. 75, 76
9:28 ................ 92
11:6 ................ 39
13:20 .............. 76
13:20–21 ........ 77

*1 Petro*
2:24 ................ 92
5:5 .................. 140

*1 Yohana*
2:1 .................. 126, 131, 130
2:1–2 .............. 127, 130
3:5 .................. 126
3:7–8 .............. 125, 130
3:8 ..... 105, 107,127, 131, 126
3:23 ................ 132
4:4 .................. 134
5:21 ................ 144